**14 FEBRUARI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

_________

## MAJADILIANO YA BUNGE

__________

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 14 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha – Mapitio ya Nusu Mwaka 2024/2025 *(Monetary Policy Statement – Mid – Year Review 2024/2025)*.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na swali la pili kwa sababu mwenye swali la kwanza ndiyo aliyewasilisha hapa kwa hiyo tunampa muda akakae kwenye kiti chake.

Tunaanza na swali namba 225, Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Na. 225

### Hitaji la Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya - Chunya

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za kujenga Ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya Chunya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya lililopo lilijengwa mwaka 1937. Kwa sasa jengo hilo ni chakavu pamoja na juhudi za ukarabati unaofanywa mara kwa mara. Aidha, Serikali imeandaa michoro na gharama za ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kipindi cha maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka 2025/2026 kimefika, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya itawasilisha maombi hayo katika mpango na bajeti unaoendelea kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatambua kwamba jengo hili ni la muda mrefu na chakavu na lilijengwa toka mwaka 1937, hivyo linahitaji kubomolewa na kujengwa upya. Sasa Serikali haioni haja ya kutoa maelekezo maalumu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iweze kutengeneza bajeti na kupeleka maombi maalumu Ofisi ya TAMISEMI ili bajeti hii iweze kutengwa na baadaye fedha hizi ziweze kutoka? *(Makofi)*

Swali la pili, pamoja na Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, bado tuna changamoto ya Ofisi ya Makatibu Tarafa. Je, Serikali ina mpango gani kujenga Ofisi ya Makatibu Tarafa katika Wilaya ya Chunya na Tanzania kwa ujumla? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekwishawasiliana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na kumpa maelekezo kupitia Katibu Tawala wa Mkoa, kuleta bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kusisitiza maelekezo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mkoa wa Mbeya ili wakati wa bajeti hii ya mwaka ujao wa fedha

2025/2026 walete maombi hayo ya kibajeti, yaingizwe kwenye bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali imeendelea kujenga majengo ya utawala nchini kote, majengo ya Wakurugenzi kwa maana ya Ofisi za Halmashauri, majengo ya Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na nyumba za viongozi hao pamoja na Wakuu wa Idara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuweka mipango kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Maafisa Tarafa katika maeneo mbalimbali ambao hawana nyumba na ofisi zao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Zaytun.

Na. 224

**Hitaji la Daraja Korongo la Oltukai – Monduli**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga daraja katika korongo la Oltukai Kata ya Esilalei – Monduli?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali imekamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa boksi kalavati ambapo gharama zilizobainishwa ni shilingi 170,000,000. Aidha, Serikali imetenga shilingi 600,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa daraja kwenye korongo la Oltukai pamoja na matengenezo ya barabara kipande korofi chenye urefu wa kilometa 2.5 ambapo barabara hiyo itachongwa na kuweka changarawe. Kwa sasa kazi hii ipo kwenye hatua za ununuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, korongo hili la Oltukai – Monduli ni hatari sana hasa kipindi cha mvua na kimeshasababisha vifo kadhaa vya watoto na akina mama wajawazito.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kufupisha hizi taratibu za kiutawala ili daraja hili liweze kujengwa kwa haraka? *(Makofi)*

Swali langu la pili, katika Wilaya ya Arumeru kuna daraja linalounganisha Chuo cha Misitu na Ngaramtoni; je, ni lini Serikali itajenga daraja hili? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Zaytun Swai kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maswali yake mawili, swali lake la kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumuagiza Meneja wa *TARURA* - Mkoa wa Arusha aweze kusimamia hatua zote za ununuzi ili ziweze kukamilika kwa wakati na ujenzi uweze kuanza mara moja katika hili eneo korofi kabisa la Oltukai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili, Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu mipango ya Serikali ya ujenzi wa daraja hili lililopo Arumeru ambalo linaunganisha Ngaramtoni, linaunga kwenda mpaka Chuo cha Misitu. Ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshaanza kufikia maeneo yote korofi na maeneo ya kimkakati kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miundombinu bora ya barabara inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumkumbusha Meneja wa *TARURA* wa Mkoa akishirikiana na timu yake ya ngazi ya Wilaya waende *site*, waone mazingira na waweze kukusanya maombi na kuyaleta kwa ajili ya kupata

fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu muhimu kabisa katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Meatu.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Mto Mwamanongu, kwa kuwa liko kwenye mpango wa fedha wa mwaka huu na limeathiriwa na mvua za *El-Nino*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Leah Komanya kwa swali lenye maslahi mapana kwa ajili ya wananchi wa Meatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa hii miundombinu ya barabara ikiwemo pamoja na madaraja yake. Nimhakikishie katika hili eneo alilolitaja, Serikali itafika kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha hiyo miundombinu ili iweze kuwanufaisha wananchi wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na. 226

**Kuongeza Kasi Zoezi la Upandaji Miti Nchini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipanga vipi kuongeza kasi ya upandaji miti ili kulinda mazingira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza kasi ya upandaji miti, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara za Kisekta na Wakala wa Huduma za Misitu na wadau wengine imeendelea kuhamasisha ushiriki wa wananchi na sekta binafsi kupitia kampeni ya kitaifa ya upandaji miti millioni 1.5 kwa kila Halmashauri nchini ambapo kwa mwaka 2023/2024 jumla ya miti milioni 226.97 ilipandwa. Kati ya miti hiyo milioni 211.81 ilistawi sawa na 76%. Tathmini ya miti iliyopandwa kupitia kampeni hii kwa mwaka 2024/2025 inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu mazingira na kuhamasisha wananchi kupanda miti kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru ambapo kwa mwaka 2024/2025 jumla ya miti milioni 150 ilipandwa na Maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar na miaka 60 ya Muungano ambapo kwa mwaka 2024 jumla ya miti 53,000 ilipandwa. Tathmini ya miti iliyopandwa kupitia utaratibu huu kwa mwaka 2024/2025 inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba kutoa wito kwa kila mwananchi na kaya kupanda miti ya aina mbalimbali ikiwemo miti ya matunda na kivuli ili kuweza kupata manufaa ya moja kwa moja yatokanayo na miti inayopandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli na kwa uhakika kabisa kampeni na uhamasishaji wa kupanda miti kitaifa imefanyika kwa kasi kubwa na miti mingi sana imepandwa katika maeneo mbalimbali ya nchi ya Tanzania. Sambamba na kwamba wadau wengi na viongozi wakuu wengi wamekuwa mstari wa mbele

katika kupanda miti hii hasa wakiongozwa na Jemedari wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye mgombea wetu pekee naye amepanda miti na ana siku maalumu ya tarehe 27 Januari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kuacha kuwapa maua yao *TBC* kwa kazi nzuri wanayoifanya katika suala hili la kuhamasisha upandaji miti Tanzania.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuunda vikosi kazi maalumu ambavyo vitaratibu na kurekodi *data* ya ile miti ambayo imeweza kumea na ile ambayo iliweza kufa na kwa sababu gani, ukizingatia nguvu kubwa sana imetumika katika kuipanda na kuilinda hii miti na hasa tija inayotegemewa katika upandaji miti ndani ya Taifa hili?

Swali la pili, Je, Serikali imejipanga vipi kuanzisha miradi ya kitaifa inayolenga kupanda miti kwenye maeneo yaliyoathirika na ambayo yako katika hatari ya kuadhibu zaidi mazingira, kwa kupanda miti katika maeneo hayo, ambapo pia kutasaidia katika kupambana na tabia hasi ya tabianchi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa kuwa amekuwa mdau mzuri wa mazingira. Kwa upande wa swali la kwanza ambalo ametaka tuwe na kikosi kazi maalumu, kikosi kazi kipo. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta tayari tunao maafisa wetu viungo ambao wapo katika kila Wilaya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaipanda na wanaishughulikia, pia wanafanya tathmini ya kujua miti mingapi imekua. Tunao pia Mabalozi wetu wa Mazingira ambao nao wanafanya kazi kubwa na nzuri sana. Ninataka nichukue fursa hii hapa kuwapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya Mabalozi wetu wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia *clubs* za mazingira, kama unakumbuka tuna Kampeni yetu ya Kusoma na Mti, ambayo tumeipeleka mashuleni, sekondari, msingi, vyuo na vyuo vikuu. Kwa hiyo, kwenye vyuo hivyo tayari kuna *clubs* za mazingira ambazo nazo pia zinafanya tathmini hiyo, lakini tunao Afisa Mazingira wa Mkoa *(REMO)* na Afisa Mazingira Wilaya *(DEMO)* wetu kwa maana ya Maafisa wa Mazingira wa Mikoa na Wilaya nao wanafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwa upande wa kikosi kazi kipo na kazi inafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia miradi, miradi yetu yote ya masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ina *component* za upandaji wa miti. Lengo na madhumuni kwanza ni kuhakikisha kwamba tunarudisha uoto wa asili. Pili, kuondoa mmomonyoko wa ardhi na tatu, ni kupambana na hali ya jangwa na ukame. Kwa mfano, miradi yetu ya *LDFS*, tunayo pia miradi ya *EBA* yote hii inakwenda katika masuala yenye nasaba ya upandaji wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe wito kwa wananchi...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, theluji katika Mlima Kilimanjaro inayeyuka kwa kasi kubwa sana na kwa kiasi kikubwa imesababishwa na uharibifu wa mazingira ambao unatokana na ukataji holela wa miti.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuipa nguvu programu ya kupanda miti katika Mlima Kilimanjaro ili kuunusuru? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwa kuwa amekuwa mdau mzuri wa masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hizi zipo na tunayo programu maalumu ya uhifadhi wa mazingira kwenye maeneo ya milima, vilima, miinuko na maeneo mengine. Kubwa nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, tuko tayari kuendeleza hii programu, lakini nimuombe na yeye pamoja kwa kushirikiana na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na maeneo ya Jimboni kwake, sisi viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais tupo tayari twende tukashirikiane kuongeza kasi ya upandaji miti katika maeneo yale ili kunusuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ninataka niwaambie tu wananchi kwamba kumekuwa kuna utamaduni wa baadhi ya watu kufanya shughuli za kibinadamu karibu na maeneo yale, mwisho wa siku tunasikia kumeungua moto, ama watu wanafuga, na kazi zingine. Kwa hiyo, ninawaomba wananchi wasifanye shughuli za kibinadamu maeneo yale, kwa lengo na madhumuni ya kuunusuru mlima ule na kuiacha theluji iendelee kuwepo ili iweze kuwa kivutio na uchumi kwa ajili ya nchi yetu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Madini. Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

Na. 227

**Uwezeshwaji Wachimbaji Wadogo**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawapatia leseni, mitambo na mitaji wachimbaji wadogo wa Jimbo la Singida Mashariki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kuwapatia wachimbaji wadogo maeneo ya uchimbaji kwa kuwatengea maeneo maalumu na kwa kupitia mchimbaji mmoja mmoja kutuma maombi Tume ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wa Jimbo la Singida Mashariki kama ilivyo kwa wachimbaji wengine wameendelea kupatiwa maeneo ya uchimbaji kupitia maombi ya mtu mmoja mmoja. Aidha, kwa upande wa maeneo yanayotengwa, Mkoa wa Singida umetengewa eneo la Mhintiri, Londoni na Sambaru kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mitambo, Serikali kupitia *STAMICO* imesaini Hati za Makubaliano *(MoU)* na kampuni wazalishaji wa mitambo ya uchimbaji hapa nchini kwa lengo la kurahishisha upatikanaji wa zana na vifaa vya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo. Kampuni hizo ni *GF Trucks*, *Apollo Heavy Equipment's* na *META*. Katika kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata vifaa *STAMICO* pia kupitia vituo vya mfano inakodisha vifaa vya uchimbaji kwa bei nafuu. Vifaa hivyo ni pamoja na *compressors* na *water pumps* (pampu za kuvuta maji).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa mitaji ya kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo, *STAMICO* imeingia makubaliano na taasisi za kifedha, zikiwemo benki za *CRDB*, *NMB*, Azania na *KCB* ili ziweze kuwakopesha fedha wachimbaji wadogo. Wizara kupitia *STAMICO* na Tume ya Madini imekuwa ikifanya semina na makongamano katika mikoa mbalimbali hapa nchini, kwa lengo la kuwafahamisha wachimbaji wadogo juu ya fursa zilizopo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru sana kwa Serikali kwa majibu yake mazuri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, mwaka 2019 vikundi vya jimboni kwangu vilipewa leseni. Vikundi hivyo ni

*Mang'onyishi Mining,* Dhahabu ni Mali pamoja na *Baraka Group,* lakini walipewa *deposit* iliyokuwa mbali sana, kwa hiyo wakawa hawana uwezo kwa sababu mtaji wao ni mdogo.

Je, wapo tayari kwenda kuongea na wachimbaji hao na kuwashauri vizuri jinsi ya kuweza kupata leseni nyingine ili waweze kupata tija?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili hawa wachimbaji wadogo kuna tozo ambayo wanatozwa kama mrahaba pale tu wanapokuwa wanatoa madini yao kwenye eneo la mgodi, wanatozwa hiyo tozo na baadaye wakienda tena sokoni wanatozwa tena kodi ya Serikali. Hii ni kama vile ni *double taxation*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapunguzia mzigo wachimbaji hawa ili waweze kupata tija katika uchimbaji wao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu kwa jinsi anavyokuwa mpambanaji makini katika kuwatetea wachimbaji wadogo wa Jimbo lake la Singida Mashariki na wachimbaji wa Singida kwa ujumla. Amekuwa pia ni balozi mzuri katika kusaidia kutatua migogoro midogo ya wachimbaji wadogo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, kama wachimbaji wadogo wamepewa eneo, lakini lipo mbali na uwezo wao wa kufika kule na kufanya uchimbaji na wanataka eneo mbadala, japokuwa ni wajibu wao kutafuta maeneo ya karibu na Wizara itakuwa tayari kuwapatia leseni kama zipo wazi, lakini nipo tayari kushirikiana naye pamoja na Afisa Madini wa Mkoa wa Singida tuangalie kama kuna maeneo mbadala wanayoweza kupewa hawa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili kuhusu mrabaha wanaokuwa *charged* mara mbili, hali halisi ipo hivi, wachimbaji wa maduara hasa kwenye madini ya dhahabu

wanachimba kwa kushirikiana na yale mawe yenye dhahabu yanapotolewa nje ya ardhi wanagawana. Wanaweza kuwa watu 20 au 30 na wanapogawana wanatawanyika, kila mtu anapeleka mahali pa kuchakatia na wanapoteza kumbukumbu na inakuwa ngumu kuwa-*trace* ili walipe mrabaha. Kwa hiyo, inabidi yale mawe ambayo ndiyo yanagawanywa ndiyo yakisiwe mrabaha ambao unalingana na makisio ya yale mawe kwa kilo, si kwa thamani yake halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapochakata kwenda kwenye masoko wanapeleka dhahabu safi iliyosafishwa na ile dhahabu safi iliyosafishwa inakuwa imeongezeka thamani na hapo ndipo Wizara inapo-*charge* tena mrabaha sahihi kwa yule ambaye amesafisha yale madini. Hivyo, ili kuepukana na changamoto hii tumekuja na utaratibu ambao unaendelea kutengenezwa wa kutengeneza maeneo ya kuchakata pamoja karibu na maeneo ya machimbo ili lile zao la mwisho ambalo ni dhahabu yenyewe liweze kuwa-*charged* mrabaha mmoja tu, ili waondokane na kero hiyo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naishukuru Serikali na mgodi wa *Barrick North Mara* kwa kukubali ku-*surrender* baada ya leseni kwa wachimbaji wadogo. Swali langu ni kwamba je, ni lini sasa Wizara ya Madini itaenda pale katika Jimbo la Tarime Vijijini na kukabidhi zile leseni kwa wachimbaji wadogo ili waanze kunufaika na madini yaliyopo katika ardhi yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza Mhehsimiwa Waitara, amekuwa pia kinara katika kutetea wachimbaji wake wa eneo la Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi anajua na tumekuwa tukifanya kazi kwa pamoja kwamba kampuni kubwa ya uchimbaji ya Barrick ipo katika utaratibu wa kuwasaidia wachimbaji wadogo ambao wameshaainishwa kufanyiwa utafiti katika

maeneo yao pia ukiachia baadhi ya maeneo yao ambayo yanaonekana hayana tija kwa uchimbaji mkubwa ili waweze kupata maeneo yenye taarifa sahihi za kijiolojia waweze kufanya uchimbaji wenye tija. Barrick ataenda mbele zaidi, atawawezesha katika teknolojia, vifaa na hata katika kutenga fedha zake za sehemu ya *CSR* ili kuinua uchimbaji mdogo ambao utasaidia pia kuondoa ile kero ya watu wanaovamia migodi yake na kusababisha maafa na vifo.

**NAIBU SPIKA:** Mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Je, ni lini Serikali itakuja kufanya utafiti Wilayani Urambo kuhusu aina ya madini tuliyonayo, kwa sababu sisi tunaamini kwamba eneo letu lina madini na sisi tunataka kunufaika nayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mama Sitta, mama yangu, kwamba kwanza ikimpendeza apite pale *GST* ili apewe kitabu cha madini yapatikanayo nchini kilichotolewa mwaka jana mwezi wa tano ili ajue kwamba tayari kuna madini yametambulika yapo kwenye eneo lake la Urambo. Kinachobaki sasa kwa sababu tuna dira yetu ya madini inaitwa *Vision 2030* ambayo dhima yake ni kufanya utafiti wa kina katika maeneo mbalimbali nchini, *STAMICO*, Wizara ya Madini kwa ujumla na *GST* wanashirikiana kufanya utafiti ili tupate maeneo yenye taarifa sahihi za kijiolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia kwa sababu maeneo yote yenye aina mbalimbali ya madini yameshabainishwa aendelee kuhamasisha wapiga kura wake na sisi tupo tayari kusaidiana naye ili waweze kubaini hayo maeneo na kufanya uchimbaji kama wachimbaji wengine.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendele, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Massare.

Na. 228

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji – Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga skimu nyingine ya umwagiliaji Itigi kwa kuwa iliyopo haifanyi kazi vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kupata gharama halisi za ujenzi wa Bwawa jipya la Itagata pamoja na kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa hili la Itagata ambalo wamelisema halifanyi kazi vizuri na swali langu lilikuwa linazungumzia ni lini Serikali itajenga skimu nyingine katika Halmashauri ya Itigi ili wananchi wangu nao wanufaike na uwekezaji huu wa Serikali ambao sasa inataka wananchi walime kilimo ambacho sio cha kubahatisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, lini bwawa lingine?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafiti zilizofanya inaonesha kwamba bwawa hili la Itagata litakwenda kufanyiwa marekebisho makubwa ili liweze kufanya kazi sahihi badala ya kuanzisha ujenzi mpya ambao unaweza

ukachukuwa muda mrefu na wananchi wakakosa hii huduma kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Gallos.

Na. 229

**Mpango wa Serikali Kuwasaidia Wakulima Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuwasaidia wakulima kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kujenga uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya kilimo kupitia sera, mikakati na programu mbalimbali ikiwemo Ajenda ya 10/30, Mpango wa Mageuzi ya Kilimo pamoja na Mwongozo wa Kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi. Mikakati yote hii inalenga kuwasaidia wakulima kuongeza uhimilivu wa sekta kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji ambacho ni cha uhakika na himilivu ili kuepuka kilimo cha kutegemea mvua;

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora za mazao kupitia *ASA* ili kuhakikisha kwamba uhakika wa upatikanaji wa mbegu unakuwepo nchi nzima;

(iii) Utoaji wa mbolea na mbegu bora kwa mpango wa ruzuku;

(iv) Uwekezaji katika utafiti wa mbegu bora na zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo *(TARI);* na

(v) Uwekezaji katika mbinu na teknolojia himilivu ikiwemo kupima afya ya udongo, uboreshaji wa huduma za ugani, kuendeleza vituo mahiri vya kusambaza teknolojia na mafunzo ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyonijibu, ili mpango huu uweze kutekelezeka Serikali ina utaratibu upi unaotumika kuwashirikisha wakulima ili kupata uelewa mpana katika suala hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyolijibu swali la msingi, ni kwamba ushirikishwaji upo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha tu kwamba wakulima wanaelewa mabadiliko mbalimbali ili kukabiliana na uhalisia wa wakati ambao hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi inajielekeza kule.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Zuena.

**14 FEBRUARI, 2025**

Na. 230

**Uhitaji wa Mbegu Bora za Minazi Mkoa wa Kilimanjaro**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mbegu bora za minazi katika Mkoa wa Kilimanjaro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuimarisha kilimo cha zao la nazi nchini ikiwemo kufufua kilimo cha zao hilo katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa kuanza kuzalisha na kusambaza miche bora ya minazi asilia aina ya *East African Tall* kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa mwaka 2023/2024 Kituo cha *TARI* – Mikocheni kilisambaza miche 300 ya minazi aina ya *East African Tall* katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Same kwa ajili ya kupanda na kuanza kuzalisha zao la nazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha *TARI* Mikocheni kinaendelea kutoa mafunzo kwa wadau wote wa zao hilo ili kusaidia ufufuaji wa mashamba na kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zao hili ni zao la biashara katika Wilaya ya Same hasa katika Vijiji vya Gonja, Mahore, Kihurio, Ndungu na maeneo ya Mnazi; je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku katika mbegu bora ili zao hili

lilimwe kwa wingi ili kunyanyua uchumi wa nchi na wananchi wa maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa zao hili linalimwa maeneo hayo na ipo minazi ya zamani ambayo ina magonjwa kiasi kwamba sasa hivi uzalishaji wake umekuwa mdogo sana; je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupambana na magonjwa haya ili angalau mazao yaliyopo yaendelee kuwa bora?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunapokea maoni ya muuliza swali kuhusu suala la ruzuku, na tafiti zitafanyika kuona namna nzuri ya utoaji wa ruzuku katika zao hili la minazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu magonjwa ambayo yanakabili minazi, Kituo cha *TARI* Mikocheni kinaendelea na tafiti za kupambana na magonjwa ambukizi ya minazi, lakini niwaombe wakulima wa zao hili, pale wanapoona dalili za mnazi mmoja katika shamba lao kuanza kuathirika, tunaushauri wauondoe haraka ili kuweka mbadala wa mnazi mwingine ili kutosambaza mnazi huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swali langu namba 331 lipate majibu ya Serikali.

Na. 231

**Kuboresha Mfumo wa Malipo ya Kahawa – Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha mfumo wa malipo ya kahawa ili kupunguza malalamiko ya wakulima kutolipwa malipo ya msimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha taratibu za usimamizi wa masoko na mauzo ya kahawa zinazoweka mazingira wezeshi kwa wakulima na wafanyabiashara kufanya biashara kwa uwazi, kuongeza ushindani, kuimarisha bei ya mkulima na kupunguza malalamiko ya wakulima, hususani ucheleweshaji wa malipo ya kahawa waliyoiuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua changamoto ya kuchelewesha malipo, kuongeza ushindani na kuongeza ufanisi, Serikali kuanzia msimu ujao wa mwaka 2025/2026 itaendelea kuboresha mifumo ya masoko kwa kupunguza muda wa mkulima kusubiri malipo ya mauzo yake kutoka wiki mbili hadi saa 48 badala ya kahawa kuuzwa kwenye mnada.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba nifanye marekebisho badala ya swali namba 331 ni swali namba 231. Nina maswali mawili ya nyongeza…

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena unasemaje?

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nauliza swali niliomba kujibiwa swali namba 331 kumbe ni namba 231 kwa hiyo naomba kufanya marekebisho hayo.

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante, *Hansard*.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa nia hii nzuri ya kuboresha huu mfumo kwamba sasa tutatoka kwenye mfumo uliopo sasa hivi kwenda kwenye saa 48. Niishukuru Serikali kwa usimamizi mzuri kiasi kwamba mwaka huu angalau vimebaki vyama saba kupata malipo yao. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa vyama hivi saba ambavyo havijalipwa malipo yake?

Swali la pili, katika kuboresha huu mfumo ambao ni kwa msimu unaokuja; je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba malipo haya, badala ya kulipwa kwa namna yanavyoenda sasa hivi sasa yatalipwa kwa mkupuo, kwamba mkulima akiuza kahawa yake basi malipo yanapokuja yalipwe kwa mkupuo tofauti na sasa ambapo anapewa *advance* na anasubiri miezi miwili anapewa malipo ya pili ambayo yanasumbua sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Kapinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na malipo ambayo hadi sasa yamechelewa, nielekeze Mamlaka ya Kahawa kuwafuatilia wafanyabiashara ambao hawajawalipa wakulima wao na zoezi hili liende haraka kwa sababu fedha hizi ambazo ni matokeo ya mauzo ya kahawa yao zinakuja kusaidia kwenye kilimo kinachofuata, kununua pembejeo na dawa kwa ajili ya kahawa. Kwa hiyo, wasimame haraka na vyama hivi ambavyo Mheshimiwa muuliza swali amevitaja malipo yafanyike haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kufanya marekebisho ya muundo mpya, huo muundo mpya tunaendelea kuuboresha, kama nilivyoeleza na kwamba kwa malipo haya kuwa ndani ya saa 48 maana yake ni kwamba mkulima huyu atanufaika na zao lake lote aliloliuza katika kipindi hicho. Hii

itawaondolea usumbufu wananchi, wale ambao wanakaa muda mrefu na wanalipwa kwa *installment* kitu ambacho sio sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, msimu wa korosho umekwisha/umefungwa lakini kuna baadhi ya wakulima zaidi ya 30 ndani ya Jimbo la Nanyumbu hawajalipwa fedha zao. Nini kauli ya Serikali juu ya jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhata, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu wa kufanya mauzo ya zao la korosho kwamba umekwishamalizika na bado kuna wananchi ambao hawajalipwa, nitoe maelekezo kwa Mamlaka ya Korosho kuhakikisha wadaiwa wote wanalipa haraka sana fedha ambazo zinadaiwa na hawa wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Nusrat.

Na. 232

**Uhitaji wa Maji Safi na Salama Sambaru - Mang'onyi**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, lini wananchi wa Kijiji cha Sambaru, Kata ya Mang'onyi Singida Mashariki watapata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Sambaru kinapata huduma ya maji kupitia skimu ya maji ya muda mrefu ya Sambaru iliyojengwa mwaka 2003 wakati kijiji hicho kikiwa na watu 3,127.

Aidha, kwa sasa kijiji hicho kina jumla ya watu 6,830 ambapo mahitaji yao ya maji yameongezeka kutoka wastani wa lita 78,175 kwa siku mwaka 2003 na kufikia lita 170,750 kwa siku mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba kijiji hicho kinapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza Serikali katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 itachimba kisima kirefu kwa ajili ya kupata chanzo cha uhakika cha maji kwa ajili ya kijiji hicho. Baada ya kisima kukamilika kazi ya usanifu wa miundombinu ya usambazaji maji pamoja na ujenzi wa mradi katika kijiji hicho utafanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Serikali kwa sababu tangu hili swali limekuja, wamekimbizana kwa kweli na nimepata hata majibu, ninajua huko kuna vitu vinaendelea tayari. Kwa hiyo, ninataka nikuhakikishie hilo jibu ni la ukweli kabisa na kuna vitu vinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maswali yangu mawili ya nyongeza, wakati Serikali inasema kwamba watachimba vile visima vitano kila jimbo, gari ambalo lilitakiwa likachimbe visima katika Mkoa wa Singida liliazimwa kwa muda kwenda Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninatamani kufahamu ni kwa nini sasa Serikali wasiongeze gari moja la ziada kwa sababu na sisi kwa nia njema tuliwaazima Simiyu, kwa nini wasiongeze gari moja lije kuongeza nguvu Singida hususani Singida Mashariki kwa sababu Jimbo la Singida Mashariki lina shida ya maji katika Kata za Kikio na Misughaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Kata ya Isuna katika Kijiji cha Ititimo kule kwetu Kidabukanje, mpaka sasa hivi kuna wakazi zaidi ya 500 pale. Nikwambie, kwa miaka kama tisa

hivi iliyopita Jimbo la Singida Mashariki kuna muda walikatazwa kuchangia kwa ajili ya kutoa nguvu zao kufanya maendeleo. Sasa hivi watu wameinuka, wanaweza kujichangisha na wakajenga hata maboma. Kwa hiyo, kuna mambo yanaendelea pale na wananchi wameinuka sana, lakini bado wana-*share* maji na fisi maana kule kwetu bado kuna fisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kule Kidabukanje, Ititimo na Isuna kule kwetu Singida Mashariki ili aende akawasikilize wale wananchi wamwambie mwenyewe na pengine ajionee maji wanayokunywa wananchi wetu kule ili sasa pengine achukue hatua? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Nusrat kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa kuwawakilisha wananchi hasa akina mama ambao ndiyo ajenda kuu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Singida, mkoa mzima ni zaidi ya shilingi bilioni 100 imewekezwa katika Mradi wa Miji 28 ambapo unachukua Singida, Manyoni pamoja na Kiomboi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote ni zaidi ya shilingi bilioni 18.3 imetengwa kwa ajili ya Mkoa wa Singida kuhakikisha kwamba maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, ni maeneo ambayo yatapitiwa katika miradi hiyo. Tunaamini kwamba zaidi ya miradi 43 inayoendelea inapokamilika, tunaanza miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa suala la kuongozana na Mheshimiwa Mbunge, Serikali siku zote dhamira yake ni kuwafikia Watanzania ambao wana changamoto ya maji

ili kwenda kujionea ukubwa wa tatizo na kuchukua hatua stahiki. Niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo ameomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu gari; Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alinunua magari zaidi ya 25 ambapo kila mkoa wana gari lao. Vilevile katika mradi wetu na Programu ya Visima 900, Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwa ma-*RM* wote kuhakikisha kwamba pamoja na kuwa na gari la Serikali, lakini tunaweza kutumia magari ya wakandarasi wengine ili kuhakikisha kwamba tunaharakisha Mradi huu wa Visima 900 ili uweze kukamilika kwa wakati. Kwa hiyo, ninamtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanyia kazi na kuhakikisha kwamba wananchi wa Singida wanapata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa hii nafasi; je, Mradi wa Maji wa Kata za Imbaseni, Maji ya Chai, Kikatiti hadi Samaria kule Maroroni, utakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana kaka yangu kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya wananchi wake. Vilevile kuhusu mradi huu, ni dhamira yetu kuhakikisha kwamba miradi yote iliyoko nchini inayoendelea inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa mara nyingine tunakutana na wakandarasi ambao wanasuasua kwa sababu za kifedha, kukosa *man power* ya kutosha na kukosa weledi wa kuendesha miradi mikubwa ambayo waliipata wakidhani kwamba wana uwezo wa kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuchukua hatua mahususi kuhakikisha kwamba miradi hii haikwami ambapo tuna uhakika wa fedha zinaendelea kutoka na wao wanaendelea kutukwamisha, tumeendelea kuchukua hatua na wengine kuwasitishia mikataba. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunapata wakandarasi ambao watakuwa na uwezo stahiki kulingana na aina ya mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kusimamia mradi huo ukamilike kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa Miradi ya Maji ya Mwika Kaskazini na Mwika Kusini upo kwenye bajeti ya mwaka huu na pia ilikuwa kwenye bajeti ya mwaka jana. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha *MUWSA* ili waweze kukamilisha miradi hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kimei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kuna miradi ambayo iko katika hatua mbalimbali. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuongea na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba wakandarasi wanalipwa na miradi inaweza kufanyika. Pia katika miradi ambayo haijaanza, tuhakikishe kwamba wanapewa *advance payment* ili waweze kuanza miradi hiyo na ili iweze kutoa matokeo ambayo yametarajiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna baadhi ya maeneo ambayo hatujatangaza. Tumeepusha kutangaza miradi mingine ambayo bila kuwa na uhakika wa fedha kwa sababu tutakuwa tunaendelea kutengeneza madeni ambayo tutaipatia Serikali mzigo mkubwa. Pia tumekuwa tukiangalia namna gani ambapo kuna maeneo ya kimkakati tutaendelea kuchukua hatua stahiki ili

wananchi waweze kupata huduma hiyo ambayo ndiyo uhai wa maisha yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Serikali ilituchimbia visima viwili virefu katika Kijiji cha Msufini kwa ajili ya kuhudumia Kijiji cha Namanguli, Msufini na Kilangalanga, lakini mpaka sasa hivi hatujapata fedha za kuendeleza miundombinu ya kugawa maji hayo.

Je, ni lini Serikali itatupa fedha ili kuendeleza kujenga miundombinu ili watu katika vijiji hivyo vitatu wapate maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri wiki hii tuliweza kukutana tukaongea, lakini ninaendelea kusisitiza kwamba jambo lako liko kwenye meza yetu tunalifanyia kazi. Pia tunaamini kwamba tunapochimba visima hiyo ni hatua ya kwanza kutupatia kujua kiu ya maji ni kiasi gani. Baada ya kujua kiu ya maji iko kiasi gani, ndipo sasa tunafanya usanifu wa kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu ya kusambaza maji kulingana na kiu ya maji ambayo tumeshaipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tunaendelea kulifanyia kazi na usanifu utafanyika na fedha zitapelekwa. Pia hakuna mradi ambao ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama ambao utakwama. Tutahakikisha miradi yote inatekelezwa vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Festo Sanga.

**14 FEBRUARI, 2025**

Na. 233

**Mradi wa Maji wa Ujuni Hadi Nkenja – Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Maji wa Ujuni hadi Nkenja - Makete utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Ujuni - Nkenja uliopo Wilaya ya Makete, Mkoani Njombe. Kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo *(intake)*, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 100,000, ulazaji wa mtandao wa mabomba umbali wa kilometa 26.4 pamoja na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 6,432 waishio kwenye Vijiji vya Ujuni na Nkenja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri na kwa jinsi ambavyo wanapambana kuhakikisha kwamba huduma ya maji inawafikia wananchi. Sisi Makete ni moja kati ya majimbo yanayoongoza kwa upatikanaji wa maji kwa wananchi, lakini kuna changamoto ambazo tunazo. Mradi huu wa Ujuni ni mradi ambao umechukua muda mrefu kidogo kutokana na changamoto, ilisainiwa miradi mitatu; Mradi wa Ujuni – Nkenja, Mradi wa Usalimwani – Mfumbi na Mradi wa Kidope – Madihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa Ujuni umefikia hatua hiyo na maji yamefika kwenye tenki...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanauliza, ni lini mtaunganisha maji kati ya tenki la zamani na tenki jipya ili waweze kupata huduma ya maji kwa wakati kabla ya kufika hiyo Juni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mradi wa Usalimwani – Mfumbi na Mradi wa Kidope – Madihani ni miradi ambayo wakandarasi hawaonekani *site*. Ipi kauli na maelekezo ya Serikali kwa wakandarasi hawa ili maji yapatikane kwa wananchi wa Makete? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia huduma ya maji kwa wananchi wake wa Makete na kwa kutupatia Serikali ushirikiano wakati tunatekeleza Ilani ya Utekelezaji wa Chama Cha Mapinduzi mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la kwanza ni kama maoni na ushauri. Ni kweli kabisa tunapokuwa tunajenga miradi ya maji haimaanishi kwamba hapo kabla hatukuwa na miradi ya maji. Tulikuwa na mtandao wa maji uliokuwa unatumika. Tunapokuja kujenga mradi mpya wakati tayari tumeshatengeneza *reservoir* (ile tenki), hakuna haja ya kusubiri kujenga mtandao mpya wakati *existing infrastructure* bado ipo. Kwa hiyo, tuna uwezo wa kuhakikisha kwamba tunaingiza katika *existing infrastructure* wakati mradi wa mtandao mpya ukiwa unaendelea ili watu waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia fursa hii kumuelekeza *RM* - Njombe kuhakikisha kwamba maji katika tenki jipya yameshajaa na nimeambiwa kwamba yanamwagikia, yaingizwe katika mtandao wa zamani na watu waendelee kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mradi wa Ujuni – Nkenja ambao umeshafikia 76%, uko katika hali nzuri na mkandarasi anaendelea na kazi vizuri bila kuwa na changamoto yoyote. Pia, Mradi wa Usalimwani – Mfumbi ambao uko 61%, mkandarasi kidogo alikuwa na changamoto na amesha-*rise certificate* ya malipo ya shilingi milioni 202 ambapo Serikali tuko katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba tunamlipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Mradi wa Kidope – Madihani; mradi huu kwa sababu ya mkandarasi kuwa anasuasua na hatupatii ushirikiano, Serikali tumeshaanza hatua za kusitisha mkataba na mkandarasi huyu ili tuweze kupata mkandarasi mwingine ambaye atakuwa yuko tayari kwenda kutekeleza miradi hii ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuchukua hatua kwa wakandarasi ambao wanaendelea kutukwamisha na sisi tunaendelea kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwawezesha wakandarasi wa ndani, lakini na wao wasichukulie kama *advantage* ya wao kutukwamisha katika kutekeleza miradi yetu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma, Mheshimiwa Issaay, ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza, ninaomba nilete salamu za Wana-Mchinga, wanaishukuru sana Serikali kwa kuwapatia maji safi na salama wakati ule ambapo Serikali ilitupatia shilingi bilioni 12.4.

Swali langu ni kwamba ile ilikuwa ni *phase one*, sasa ni lini Serikali itatupatia *phase two* ili kuhakikisha kwamba Wana-Mchinga wanapata maji safi na salama kwa sehemu iliyobakia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwepo Lindi, nilikutana na Mheshimiwa Mbunge na tulijadili. *Phase* ya kwanza kweli Serikali imefanya kazi kubwa sana kwa kazi ambayo ilifanywa na Mheshimiwa Mbunge kwa kuomba fedha hizi shilingi bilioni 12.4 Serikalini. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile alinieleza kuhusu awamu ya pili na Serikali tumeshalipokea na tuko kwenye mchakato wa kutafuta fedha ili awamu ya pili ikaanze na wananchi wa Mchinga katika maeneo ambayo yamebaki wapate huduma ya maji safi na salama na kweli kabisa ninakumbuka kuna eneo ambalo watu wa kule hawana kabisa maji. Sisi tumelichukua kwa uzito wake. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tuko kwenye hatua nzuri kabisa kuhakikisha kwamba tunapata fedha ili wananchi hao wapate huduma ya maji safi na salama baada ya kutekeleza mradi huu wa awamu ya pili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Serikali tayari imechimba visima vitano katika Jimbo la Mbulu Mji kwa programu yake ya majimbo yote nchini na ni miezi sita sasa; je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza miundombinu hiyo ili wananchi waanze kupokea maji kwenye hivyo visima vitano katika Jimbo la Mbulu Mji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Programu yetu ya Visima 900, hatua ya kwanza tunachimba visima na tuliwekeana muda kufikia Disemba tuwe tumeshachimba visima vyote. Mpaka Disemba tulikuwa tumeshakamilisha kuchimba visima vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ni kufanya usanifu na kujenga *point source* ili wananchi waweze sasa kuanza kupata huduma ya maji safi na salama. Tumeshapeana *deadline* ma-*RM* wote nchini, itakapofika mwezi wa tatu visima vyote viwe vimejengewa miundombinu ya kuchotea maji ili wananchi waweze kuona maji yanatoka katika mabomba yao, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, kwanza, ninakupongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ziara yako katika Jimbo la Kishapu. Miradi uliyoiona na kuizindua inaendelea vizuri, lakini Kata za Mondo, Sekebugoro na Mwasubi ni kata ambazo bado zina taabu kubwa ya maji. Upembuzi wa kina na upembuzi wa awali umeshafanyika ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.4 zinahitajika. Sasa ni lini Serikali inaenda kuleta hizi fedha ili wananchi waondokane na adha kubwa ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Butondo anafanya kazi nzuri sana katika Jimbo la Kishapu, lakini vilevile tulifanya naye ziara katika jimbo zima. Tulitembea katika kata zote ambazo amezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo amevitaja, tunaenda kuchukua maji kutoka kwenye gridi ya Maji ya Ziwa Victoria ambapo maji hayo yanasimamiwa na *KASHWASA*. Vilevile miundombinu yake inahitaji fedha nyingi kiasi ambapo kwa sasa Serikali inatafuta pesa kidogo kidogo za kuanzia ili tuanze na tuwe na uhakika kwamba kila tunachokifanya basi kinakuwa kinaleta *impact* kwa wananchi. Kikubwa ni kwamba tunatafuta fedha ili tuanze ili baadaye katika mwaka wa fedha ujao tutaweza kukamilisha, lakini kwa sasa tuna pesa kidogo.

Kwa hiyo, ninamtoa hofu Mheshimiwa Butondo, tunalifanyia kazi na sisi tunaguswa na changamoto ya wananchi wa Kishapu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyotaja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuja kwenye jimbo langu. Kuna Visima vya Qaloda, Muslur, Endagaw na Bisigeta vimechimbwa, lakini bado haujatuletea fedha ya kumalizia kujenga matenki. Je, ni lini unatuletea fedha hizo ili matenki yakajengwe na wananchi wakapate maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu swali lake na hoja yake alikuwa ameshaileta Wizarani kwa ufuatiliaji, ninaomba nitumie fursa hii kumuomba tukitoka hapa niweze kuifuatilia, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Basi ahsante, atarudi tena Wizarani huko huko. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mkenge.

Na. 234

**Hitaji la Boti kwa Jeshi la Polisi – Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itanunua boti na vifaa kwa Jeshi la Polisi Bagamoyo ili kudhibiti biashara za magendo na wahamiaji haramu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia bajeti yake ya mwaka wa fedha 2023/2024 ilitenga fedha kiasi cha shilingi 4,500,000,000 ili kununua boti 11 kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi katika kufanya doria maeneo ya baharini na ziwani. Boti sita zimeshawasili na zipo bandarini na taratibu za kutizoa zinaendelea. Pindi zikikamilika zitakabidhiwa Kikosi cha Polisi Wanamaji kwa ajili ya doria ya kudhibiti matukio ya uhalifu kwenye maji na maeneo ya Wilaya ya Bagamoyo yatafikiwa na kuhudumiwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaipongeza Serikali kwa kununua boti hizi kwa ajili ya doria katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi, katika hizi boti sita ambazo zimewasili basi angalau moja iwe *stationed* pale Bagamoyo kwa ajili ya kufanya kazi ya kupunguza magendo pamoja na wahamiaji haramu katika Pwani ile ya Bagamoyo mpaka Pangani – Tanga, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kikosi cha Polisi Wanamaji kipo Kanda ya Kusini, Kaskazini na Kanda ya Upande wa Kigamboni. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa upande wa Kaskazini iko Wilaya ya Bagamoyo, kwa hiyo na boti moja itakaa upande huo kwa ajili ya kudhibiti uhalifu katika eneo la Bagamoyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, je, ni lini Serikali itanunua samani za kisasa katika vituo vya polisi vilivyopo katika Jimbo la Kalenga? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli viko vituo vya polisi ambavyo havina samani na vya Wilaya aliyosema, pia tutalichukua tuliweke kwenye mpango wa kulitengea fedha kwa ajili ya kununua samani, tayari kwa matumizi katika ofisi hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ndaisaba.

Na. 235

**Hitaji la Gari la Zimamoto – Ngara**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la zimamoto Wilayani Ngara hususani katika Mradi wa Rusumo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umeme wa Rusumo ulianzishwa kwa ushirikiano wa nchi tatu ambazo ni Tanzania, Rwanda na Burundi na unatekelezwa kupitia mikopo iliyotolewa na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshiriki katika hatua zote ili kuhakikisha mradi huo unakuwa salama. Katika mradi huo, limenunuliwa gari moja la kuzima moto aina ya *Mercedes Benz Acros 2036 (4x2)*

lenye ujazo wa lita 5000 za maji na lita 500 za *foam*. Aidha, gari hilo linatarajiwa kupokelewa na kukabidhiwa ifikapo mwezi Julai, 2025, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunipa majibu mazuri katika nyakati nzuri sana kwa sisi wanasiasa na nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa gari hili limeletwa mahususi kwa ajili ya Mradi wa Rusumo, na kwa kuwa mahitaji ya magari ya zimamoto ni makubwa, ukizingatia wilaya ni kubwa. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inatuletea gari lingine la ziada kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Ngara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa watumishi wa Jeshi la Zimamoto Ngara ni wachache hawazidi watatu, na kwa kuwa ujio wa hii mitambo unahitaji askari wengi zaidi wa zimamoto. Ni nini mkakati wa Serikali wa kuongeza idadi ya askari wa zimamoto Ngara ili waweze kutumika nyakati za majanga? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mkubwa wa magari haya ya zimamoto katika Wilaya yake ya Ngara. Pia pongezi alizozitoa ziende kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mahitaji ya gari nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imeagiza magari 150 kwa ajili ya zimamoto wilaya zote hapa nchini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge Wilaya hii ya Ngara pia mtapata gari nyingine kwa ajili ya zimamoto na uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili ni kweli kuna baadhi ya ofisi ambazo zina uchache wa watumishi lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetangaza nafasi za kazi hivi sasa, watakapoajiriwa basi tutaangalia pia watumishi wengine waende kwenye Wilaya ya Ngara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Wilaya ya Mbogwe imekuwa kubwa je, lini mtatupatia gari la zimamoto maana shoti zinatokea, nyumba za watu zinaungua, na wanapata hasara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujali imeagiza magari 150 kwa ajili ya zimamoto katika wilaya zote nchini, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe gari la zimamoto mtalipata pindi litakapowasili hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Ningependa kufahamu ni lini gari ambalo niliahidiwa humu Bungeni litafika Mkoa wa Songwe? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, magari haya yameshaagizwa na yameshalipiwa. Kwa hiyo, yatakapofika hapa nchini, yatagawanywa na kusambazwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na eneo la Mkoa wa Songwe ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Bupe.

Na. 236

**Kukarabati Meli Zilizopo Ziwa Tanganyika**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati meli katika Ziwa Tangayika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeanza ukarabati wa meli zilizopo Ziwa Tanganyika. Taarifa za ukarabati huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ukarabati wa meli ya MV Liemba; mradi huu ulianza rasmi tarehe 13 Julai, 2024 baada ya mkandarasi kulipwa malipo ya awali kiasi cha dola za Kimarekani 1,890,405.31. Mradi huo unaogharimu kiasi cha dola za Kimarekani 13,192,850.00 na unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi 24 kwa mujibu wa mkataba husika hivyo utakamilika tarehe 13 Julai, 2026.

(ii) Ukarabati wa meli ya MV Mwongozo; mchakato wa kumpata mkandarasi wa kuikarabati meli ya MV

Mwongozo uko katika hatua za mwisho ambapo tayari mkandarasi *M/S Songoro Marine* ameshapatikana na kwa sasa taratibu za kuandaa mkataba zinaendelea. Mradi huo ambao utagharimu dola za Kimarekani 4,000,000 umepangwa kutekelezwa ndani ya miezi sita .

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa meli ya MT Sangara; mradi huu sasa umefikia 98% na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2025. Mradi huo umegharimu dola za Kimarekani 3,606,595.00.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa niipongeze sana Serikali kwa hatua iliyofikia ya ukarabati wa meli kufikia 98%. Hii ni habari njema kwa mikoa hii mitatu, Mkoa wa Katavi, Rukwa na Kigoma ni habari njema sana tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua aliyofikia. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika ni uchumi na ni ajira kwa mikoa hii mitatu. Maisha yetu yote tunategemea Ziwa Tanganyika, lakini ziwa hili limekuwa kimya sana usiku utakuta ni giza tupu, ni giza totoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa ina mpango gani madhubuti wa kuhakikisha kwamba ziwa hili linakuwa na tija kwa wananchi hawa wa mikoa mitatu, kwa sababu ziwa hili linaunganisha hata nchi tatu za Burundi, Congo, Zambia na Tanzania. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba ziwa hili linatija kwa wananchi hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Bupe kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa na kwa kweli pongezi hizi zinatakiwa zimfikie, kwa sababu katika historia ya nchi yetu Ziwa Tanganyika ndiyo linafanyiwa mageuzi makubwa ya kiuchumi kuliko wakati mwingine wowote na hii imetokana na ukweli kwamba ndani ya

Ziwa Tanganyika Tanzania inamiliki karibu 41% ya ziwa lote hivyo manufaa yake lazima yaonekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ameuliza mchakato ambao Serikali imefanya wa kunufaisha ziwa hilo kiuchumi, kiajira na usalama. Naomba nizungumze mambo machache kuhusiana na hoja hii ya pili. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tangu alipoingia madarakani mwaka 2021, yapo mambo machache naweza kuyataja kati ya mengi aliyoyafanya yanadhihirisha kwamba anaamini, anaelewa, anazingatia na anaishi kwa kutambua Ziwa Tanganyika ni muhimu kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kama nilivyosema tayari Serikali imekarabati meli tatu; MV Mwongozo, MV Liemba na MT Sangara. Meli hizi zilikuwa hazifanyi kazi kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali inajenga meli mbili kubwa kwa sasa. Meli ya kwanza ni meli ya mizigo, hii itakuwa na uwezo wa kubeba tani 3500; katika nchi yetu hatukuwahi kujengewa meli kubwa kama hii. Pili, ni meli ya mizigo ambayo tunategemea itaweza kubeba abiria 600 pamoja na tani 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais wetu amesaini mkataba wa kujenga kiwanda kikubwa cha kujenga na kukarabati meli ambacho kitatumika siyo tu kwa meli zetu Tanzania, lakini pia kwa meli za nchi jirani ambazo zinazunguka katika ziwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi Mheshimiwa Rais na Serikali yake ya Awamu ya Sita, wamefanya ukarabati mkubwa wa bandari zote kuanzia Kasanga, Kabwe, Kalema na Kigoma; yote haya yanadhihirisha anaelewa na anaamini kwamba Ziwa Tanganyika ni uchumi, ni ajira na ni usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ambao imekwishaanza kujengwa, sasa hivi kutoka Mpanda mpaka Kalema, na hii imekuwa ni kilio cha muda mrefu sana cha Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa huo

kuunganisha miundombinu hiyo ya ziwa pamoja na miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hivi ninavyozungumza ukarabati wa reli inayotoka Kaliua hadi Mpanda uko 40%. Miundombinu hii inaunganisha Bandari ya Dar es Salaam na Ziwa Tanganyika, na kama haitoshi, kwa kumalizia, kwa sababu tunazungumzia usalama, hivi ninavyozungumza tupo katika hatua za mwisho kama Serikali kuandaa makabrasha kwa ajili ya kutangaza zabuni ili kupata boti nne za uokoaji; mbili Ziwa Tanganyika, moja Ziwa Nyasa na moja kwa Ziwa Victoria.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa baada ya majibu haya mazuri kuna swali la nyongeza tena? Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri ni muda mrefu Ziwa Tanganyika hakukuwa na usafiri na tumechoka kupoteza ndugu zetu wanaotumia usafiri usio rasmi. Wakati mnasema hapa, mlisema kwamba ukarabati utaendana na kuleta meli mpya pamoja na kutengeneza chelezo. Lini meli mpya hizo zitakamilika ili tuache kupoteza ndugu zetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, naomba kurejea, kwanza tuungane na Mheshimiwa Bupe aliyepongeza kwa kiasi kikubwa sana mpango huu ambao tumeuzungumza, kwa sababu kushukuru ni kuomba tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa, anazungumza ni lini? Ni mara baada ya kukamilisha taratibu za awali za kimikataba tutaanza ujenzi na ukarabati kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, tokea meli zinazomilikiwa na Serikali za MV Clarias na Butiama kupelekwa matengenezo kumekuwa na shida kubwa sana ya usafiri kati ya Bandari ya Nansio kwenda Mwanza na inasababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi na abiria kwa ujumla wake. Lini sasa ukarabati huu utakamilika? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Mbunge katika kuona umuhimu mkubwa wa meli zetu katika Ziwa Victoria hususani ambazo zinakwenda kule Nansio. Nimhakikishie kwamba tumeanza taratibu za awali kwa upande wa meli ya MV Clarias kama alivyozungumza, tunapozikamilisha, tutaanza matengenezo. Hata hivyo, kwa upande wa MV Butiama tayari tumekwishaanza matengenezo kulingana na maelekezo ya *TASAC* ambaye ndiye mdhibiti na tunategemea ndani ya miezi mitatu hadi minne hii tutakuwa tumekamilisha matengenezo na usafiri utaweza kurejea kama ilivyokuwa awali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

Na. 237

**Ushiriki wa Wabunge wenye *CPA* kwenye Kamati Kuchukuliwa kama *CPE Hours***

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, lini Wabunge wenye sifa ya *CPA* ushiriki wao kwenye Kamati za *LAAC, PIC, PAC* na Bajeti utachukuliwa kama *CPE hours*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Mafunzo Endelevu ya Kihasibu Tanzania *(Continued Professional Development- CPD Guideline)* uliidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya *NBAA* na kuanza kutumika rasmi Julai 1, 2020. Mwongozo unatambua mafunzo endelevu rasmi yaani uso kwa uso au ya kielektroniki na mafunzo endelevu yasiyo rasmi ikiwa ni pamoja na kushiriki mikutano ya kiufundi katika tasnia ya uhasibu na ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufuata mwongozo huo na kwa kuzingatia muda unaotumiwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa ushiriki wa mikutano ya Kamati za Bunge na hasa zile zinazohusu masuala ya uhasibu au ukaguzi kama *LAAC, PIC, PAC* na uchambuzi wa Bajeti ya Serikali, saa zinazotumiwa na Wabunge wenye *CPA* zinatambuliwa kama ni mafunzo endelevu *(CPD hours)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ambaye ni mwanachama wa *NBAA* ataingia kwenye akaunti yake, atapandisha ratiba ya kikao husika na uthibitisho wa mahudhurio katika mkutano husika ili saa zakezi kuhesabiwa. Hivyo, ni jukumu la mwanachama mwenyewe kuingia kwenye mfumo, na siyo mtu mwingine *(third party)* na kutoa uthibitisho huo kwenye mfumo wa *NBAA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa majibu ambayo binafsi nimeshiba, nimeridhika na wale Waheshimiwa Wabunge wote wenye *CPA,* nina uhakika watakuwa wameridhika na majibu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi au swali moja tu, ni kwamba kwa kawaida kila mwaka Bodi ya *NBAA* huwa inafanya mkutano wa wahasibu wote wenye sifa za *CPA,* kwa mfano mwaka huu inafanyikia Mwanza. Je, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Bunge mpo tayari kuwalipia Waheshimiwa Wabunge kila mwaka wenye sifa ya *CPA?* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za Waheshimiwa Wabunge kushiriki mafunzo na kushiriki shughuli zake yameainishwa, punde taratibu hizo zitakapokuwa zimefuatwa sisi kama Wizara hatutakuwa na tatizo la kushirikiana na Bunge kutekeleza hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhe. Dkt Kikoyo, ajiandae Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na nishukuru kwa majibu ya Serikali, je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha kwamba wahasibu pamoja na wanasheria na fani nyingine zote ambazo zinahitaji kupata mafunzo, kwa Waheshimiwa Wabunge ambao tupo Bungeni na kutumia muda tunaotumia kwenye Kamati zetu kama sehemu ya mafunzo kwenye taaluma zetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haipingani na maoni ambayo yametolewa na Mheshimiwa Mbunge, niseme tu tutashirikiana na Ofisi za Bunge, kuwa tunaratibu masuala ya aina hiyo kama ambavyo yamefanyika mara kwa mara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nami niwapongeze sana Serikali kwa majibu yale ya msingi yaliyotolewa kuhusu hoja ya wahasibu, wahandisi, wanasheria wanaobeba jukumu la kulipa *annual subscription* katika taasisi zao za kitaaluma na hizi zimekuwa zikilipwa kwa watumishi wa umma wenye *professional* kama hizi za wanasiasa ambao ni Waheshimiwa Wabunge.

Je, Serikali hamuoni sasa ni wakati wa kuwalipia Waheshimiwa Wabunge hizi *annual subscription* katika taaluma zote hizo nilizozitaja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo zuri lakini kwa kuwa halijafanyiwa kazi kwa namna hiyo tulipokee na kwenye orodha yake awaongeze na wachumi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kuna Waheshimiwa Wabunge ambao hawana *CPA* lakini wametumika kwenye hizi Kamati ya *LAAC, PAC* kati ya miaka 10 mpaka 15 na walikuwa wanapata mafunzo ya *CAG* ambayo pia ni mafunzo ya kiuhasibu kwa hapa. Waheshimiwa Wabunge hawa ambao wamedumu kwa miaka hii yote Serikali haioni kwamba na wenyewe waweze kupatiwa *Honorary CPA? (Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani na lenyewe si jambo baya wanaweza wakapata heshima, naamini watu kutunukiwa heshima huwa kuna vigezo, vikishazingatiwa ni jambo ambalo huwa linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkumbuka kaka yangu mpendwa na Mungu amrehemu *Engineer* Kwandikwa alizoeleka kuwa ni *engineer* baada ya kuchangia sana kwenye sekta ya *TANROADS,* lakini yeye kitaaluma hakuwa *engineer* na alipata heshima ile. Kwa hiyo, naamini ni jambo zuri, taasisi zetu zitaendelea kuangalia watu wanaostahili kupata heshima hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni sababu gani inayosababisha mafunzo ya *CPA, ACCA, CFA* kukosa taasisi maalumu ya Serikali ya kufanya *training* na badala yake wanaenda kufanya *training* za watu binafsi na ambazo hazipo rasmi. Ni nini sababu ya Serikali kutokuanzisha mfumo rasmi wa kuwa na mafunzo ya *CPA, CFA, ACCA*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilianza kwa utaratibu huo, lakini katika kipindi cha hivi karibuni nadhani mwaka 2024 tumerekebisha sheria ambayo inahusu taasisi hizi. Tunaamini tunapokwenda, maboresho yataendelea kufanyika ili masuala ya mafunzo kama ilivyo katika tasnia zingine yawe kwa Serikali na kwa sekta binafsi kama ambavyo imekuwa ikifanyika katika maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

Na. 238

**Kuboresha Ofisi na Makazi ya Wanajeshi**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED K.n.y. MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali kuboresha ofisi na makazi ya Jeshi la Wananchi nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2025/2026 wa kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuboresha mazingira ya kazi. Katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara inaendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa – Kikombo, Dodoma, uboreshaji na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika vikosi, vyuo na shule. Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mpango wa nyumba 10,000 ambapo hadi sasa

jumla ya nyumba 6,064 zimejengwa katika mikoa mbalimbali nchini. Vilevile Wizara inaendelea na ujenzi wa nyumba 3,936 zilizosalia kulingana na upatikanaji wa fedha za maendeleo. Aidha, Wizara inaendelea na ukarabati wa nyumba 6,064 katika maeneo mbalimbali ya Jeshi la Wananchi, ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi Msalato - Dodoma, uboreshaji wa Hospitali ya Kanda MH Mwanza na ujenzi wa mabweni ya maafisa na askari katika vikosi na viteule mbalimbali, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile bado kuna shida ya Wanajeshi wetu hasa katika eneo la makazi, na kwa vile Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania limekuwa likifanya vizuri ndani ya mipaka ya nchi yetu lakini pia limekuwa likifanya vizuri nje ya mipaka ya nchi yetu. Hivi Serikai haioni sasa haja ya kuharakisha programu hii ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa Wanajeshi wetu?

**NIABU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Bakar kwa kufuatilia kuhusu maslahi ya wanajeshi wetu na kama nilivyosema kwenye majibu ya swali la msingi huu mpango wa kujenga nyumba 10,000 na nyumba ambazo zimeshajengwa 6,064 na hizi zilizobaki 3,936 ni kipaumbele cha Serikali kuendelea kujenga nyumba hizi ili kuweka mazingira mazuri ya askari wetu kwenye maeneo ya makazi wanayoyahitaji, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Musoma Mjini niliwahi kuleta hoja ya wananchi wanaokaa kwenye eneo la Jeshi la Makoko na ninashukuru kwamba Serikali iliweza kutuma timu yake ikaenda kuangalia uhalisia. Sasa ningependa kufahamu, baada ya kuwa mmeenda na mmeangalia, uamuzi wa Serikali ulikuwa ni upi kuhusiana na wale wananchi wanaokaa kwenye eneo lile na uki-*consider* kwamba mahitaji ya shule ni muhimu sana kwa wale wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mathayo, jambo hili amekuwa akilifuatilia na mimi nilihusika kipindi nikihudumu katika hii Wizara, lakini niipongeze Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya hili ambalo amelisema na yenyewe ni hatua, kwanza, kutambua changamoto. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa hatua hii ambayo imefikiwa hata hizo hatua nyingine muhimu ambazo zinahitaji kufanyika ili kutatua mgogoro huu zitafanyika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Na. 239

**Ujenzi wa Daraja la Sanza**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Daraja la Sanza – Manyoni utaanza baada ya mkandarasi kupatikana tangu Februari, 2024?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa Daraja la Sanza. Kwa sasa Serikali iko katika hatua ya kukamilisha taratibu za kusaini mkataba wa ujenzi. Mara baada ya mkataba kusainiwa kazi za ujenzi zitaanza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya matumaini ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka *Manyoni East* inaenda Heka - Sanza - Chali Igongo inakuja hapa Dodoma Mjini na hii ni barabara muhimu sana *incase* ikitokea kuna *emergence* kati ya barabara ya kutoka Manyoni kuja Dodoma. Sasa nini mkakati wa Serikali wa kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kikao cha mkoa cha *Road Board* kilipitisha azma ya kuhamisha barabara ya kutoka Kitinku – Makanda - Chemba - Kondoa kuitoa *TARURA* kuipeleka *TANROADS*. Je, ni lini sasa *TANROADS* wataanza kuihudumia hii barabara? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Dkt. Chaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo aliyoitaja kwa maana ya kuijenga kwa kiwango cha lami ndiyo barabara ambayo inapita kwenye hilo Daraja la Sanza na inaanzia hapa Bihawana - Chali Igongo – Sanza - Heka hadi Manyoni. Hivi sasa tunapoongea tumekamilisha taratibu zote ili iweze kufanyiwa

usanifu, labda tu niwaagize Mameneja wa Mkoa wa Singida na Dodoma wakamilishe ili tunapoanza ujenzi tuwe tunaendelea pia na usanifu wa hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Kitinku hadi Kondoa lini itaanza kukarabatiwa na *TANROADS*. Ni taratibu, kama ni *Road Board* ya Mkoa itaenda *RCC* tukishaipokea na kuikagua na kuona inakidhi vigezo ndiyo tutakapoipandisha daraja na kama itakuwa imepandishwa daraja wakati bajeti imepita, basi bajeti iliyokuwa imepangwa na wenzetu wa *TARURA* itabidi iweze kusimamiwa na *TANROADS,* lakini kama itakuwa imepanda basi maana yake sisi tutaanza kuihudumia kama itakuwa imekidhi vigezo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kibajaji.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kutupatia pesa kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya *Ntyuka Junction - Mvumi Mission* - Kikombo. Swali langu, je, ujenzi utaanza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunavyoongea sasa hivi mkandarasi alishapatikana, tulishasaini mkataba na changamoto ilikuwa ni kumlipa malipo ya awali. Ninavyoongea sasa hivi ameshalipwa fedha yote ya awali 10% na muda wowote anatakiwa awepo *site* kuanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Rungwe kuna barabara ambayo ni muhimu sana, inasafirisha mazao kwa wingi. Barabara hiyo inaanzia Kiwira – Isangati - Mbalizi kwenda mpaka Ileje, Mkoani Songwe. Je, ni lini Serikali itaanza kuijenga barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, si mara ya kwanza kuulizia kuhusu hii barabara na ni kipande ambacho hakijasanifiwa tu, kutoka Kiwira - Igogwe hadi Isangati kwa maana ya Isangati kwenda Mbalizi na Isangati kwenda Ileje, usanifu uko hatua za mwisho na tunavyoongea sasa hivi hicho kipande cha Isangati hadi Kiwira kimeingizwa kwenye mpango ili kianze kufanyiwa usanifu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege.

Na. 240

**Malipo ya Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Barabara ya Bulamba – Kisorya**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha malipo ya wananchi waliopisha ujenzi wa mradi wa Barabara ya Bulamba - Kisorya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha shilingi bilioni 2.384 kimelipwa kama fidia kwa wananchi 833 waliopisha ujenzi wa Barabara ya Bulamba – Kisorya ambao walistahili fidia kwa mujibu wa sheria. Wananchi ambao bado hawajalipwa fidia ni wale ambao wapo katika eneo la hifadhi ya barabara lililoongezwa kutoka meta 22.5 hadi meta 30 kila upande kulingana na Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009. Kwa sasa uchambuzi wa kina unafanyika ili kubaini ni barabara zipi kweli zinahitaji upana wa eneo la hifadhi ya

barabara wa meta 60 kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na hapo baadaye na hii ni kwa barabara zote. Baada ya kukamilisha zoezi hili taarifa ya Serikali itatolewa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi niulize swali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuwalipa fidia wananchi wangu hawa. Kwa vile bado baadhi ya wananchi wanadai kwamba hawajalipwa fidia hii na wapo katika eneo ambalo limelipwa. Je, ni lini Serikali itakutana nao mmoja mmoja ili kuona namna ya kuwasaidia? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna utaratibu ambao tunapolipa fidia tunaunda kamati ambazo Mwenyekiti anakuwa ni Mkuu wa Wilaya husika na Katibu anakuwa ni Meneja wa *TANROADS* na wajumbe huwa ni wananchi ambao barabara huwa inapita. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuwasiliane ili tuone kitu gani kimekwamisha kwa sababu Kamati ya Malalamiko kwa wananchi wote ambao wanakuwa wamepunjwa au wanalalamika huwa ipo ili tuweze kuona ni kitu gani kimekwamisha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kumlipa mkandarasi wa Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda kiasi cha shilingi bilioni 4.7, wiki mbili sasa zimepita bado hajarejea *site*. Nini

mpango kazi wa Serikali kumsimamia mkandarasi huyu ili aweze kuendelea na kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maelekezo tu nimpe Meneja wa Mkoa wa Njombe kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu *CCECC* anarudi *site* kwa sababu tayari ameshalipwa. Kwanza, akafanye ukarabati kwa barabara ambayo inapitika, lakini aendelee na ujenzi ambao ulikuwa umesimama, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, wananchi wa Iboya, Kata ya Ihanda wamesubiri kwa muda mrefu sana malipo ya fidia baada ya kupisha upanuzi wa barabara. Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Iboya ni kituo ambacho tunategemea kitakuwa cha muhimu sana kwa Mji wa Tunduma ikiwa ni pamoja na kupunguza fidia. Thamani ambayo wanadai kama sikosei ni shilingi bilioni 4.9. Sasa hivi tunavyoongea, Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Fedha wako kwenye hatua za mwisho kuhakikisha kwamba wanalipwa ili kituo hicho kianze kujengwa kwa ajili ya kusaidia kupunguza msongamano wa magari katika Mji wa Tunduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Ni lini Serikali itajenga barabara ya Kibosho kwa Raphael mpaka *International School* ambayo ni lango la kuingia watalii Jimbo la Moshi Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara aliyoitaja tumekasimiwa kuisimamia na tunachoweza kufanya kwa sasa na wenzetu wa *TARURA* kwanza ni kuifanyia usanifu halafu tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami ili kuboresha shughuli za utalii katika Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ni kipindi cha wageni, maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha ni viongozi kutoka Wizara hiyo; Ndugu Leonard Mkude - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Ndugu Meshack Anyingisye - Kamishina wa Bajeti na Ndugu Johson Nyela - Kamishina Uchambuzi wa Sera. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni kumi wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao ni watumishi wa Kituo cha Afya Kibakwe, Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 57 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa - Naibu Waziri Madini ambao ni viongozi wa CCM ngazi ya Kata kutoka Jimbo la Longido, Mkoa wa Arusha wakiongozwa na mke wake, Ndugu Agnes Kiruswa. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis - Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Mwenyekiti wa CCM Tawi la Bambi, Mkoa wa Kusini Unguja Zanzibar pamoja na Maafisa Viungo wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano. *(Makofi)*

Wapo wageni 54 wa Mheshimiwa Profesa Ndakidemi ambao ni wanawake Wakatoliki Olasiti kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambaye ni mwanachama wa CCM kutoka Kalenga, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ambaye ni Ndugu Mfaume Masubo - Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Felista Njau ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, Muswada huo ninauelekeza kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(The National Health Insurance Fund (Amendment) Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Muswada huu ninauelekeza uende Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Muswada huu ninauelekeza uende Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapendekezo ya nyongeza ya mapato na matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 945.7 kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njenza kwa kuujadili kwa kina muswada huu na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Aidha, nitoe shukrani zangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wataalamu wake, pamoja wataalamu wa Wizara ya Fedha kwa kuuandaa muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea na juhudi zake za kutafuta fedha kwa ajili ya kuwaletea Watanzania huduma za kiuchumi na kijamii pamoja na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Hadi Disemba, 2024, Serikali ilikuwa imepokea shilingi bilioni 460 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika *(AfDB)* na shilingi bilioni 130 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Fedha za *African Development Bank* zilikuwa zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024 zikachelewa kupatikana kwa wakati, hivyo zikaingia Mfuko Mkuu wa Serikali mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nusu ya pili ya mwaka 2024/2025, Serikali inatarajia kupokea zaidi ya shilingi bilioni 356 kutoka *IMF* ambazo nazo siyo sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Fedha hizi kutoka *IMF* zinajumuishwa kwenye bajeti ya mwaka 2024 kwa kuwa majadiliano yake yalikamilika katika kipindi ambacho mapendekezo ya bajeti yalikwisha kukamilika, hivyo hazikujumuishwa kwenye bajeti ya mwaka 2024/2025. Hivyo basi kwa mwaka 2024/2025 Serikali ilipata ziada ya jumla ya shilingi bilioni 945.7 ambazo siyo sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha hizo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa

fedha 2024/2025 na kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 137(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Serikali inawajibika kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya kuomba ridhaa ya Bunge ya nyongeza ya bajeti. Kufuatia hali hiyo, inapendekezwa kuongeza Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/2025 kwa kiasi cha shilingi bilioni 945.7 hadi shilingi bilioni 50,291.4 kutoka shilingi bilioni 49,345.7 iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za nyongeza ya bajeti kiasi cha shilingi bilioni 945.7 zimeelekezwa kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwepo za sekta ya elimu na afya, taasisi za utalii na utekelezaji wa programu mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo huu umezingatia maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na nguvukazi yenye ujuzi kwa kuhakikisha utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu ya amali ni kwa vitendo. Pia fedha hizi zitaendelea kuhakikisha kuwa utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwa jamii ni endelevu. Vilevile mgawanyo wa fedha hizo umezingatia mapendekezo ya sekta tajwa, makubaliano kati ya Serikali na washirika wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 21 – Hazina; tunapendekeza kupeleka shilingi bilioni 325 ambazo zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; shilingi bilioni 135.4 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kugharamia mahitaji ya mitaala mipya ya sekta ya elimu, ikiwemo ujenzi wa shule za sekondari za amali, upatikanaji wa vifaa na walimu. Aidha, fedha hizi zitagharamia ukamilishaji wa ujenzi wa vyuo vya *VETA*, ujenzi wa Maktaba ya Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa – *MUCE,* ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Nelson Mandela – Arusha, ujenzi wa jengo la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Mkoani Mwanza na ujenzi wa jengo la Maktaba – Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Afya; shilingi bilioni 53.7 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande kwa Fungu 056 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; shilingi bilioni 173.7 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miundombinu katika sekta ya afya na elimu, pamoja na kuiwezesha *TARURA* kukarabati miundombinu ya barabara na madaraja yaliyoathiriwa na mvua za masika na hivyo kuweza kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Maliasili na Utalii; shilingi bilioni 260.7 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara katika hifadhi za Taasisi za Utalii za Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha; kwa kuwa fedha hizo hazikuwa sehemu ya bajeti ya mwaka 2024/2025 iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, nawasilisha hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu ili liweze kuridhia mapendekezo ya Serikali ya kuongeza mfumo na ukomo wa bajeti kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 2. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kutimiza matakwa ya Ibara 137(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu

Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kuhusu Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Nyongeza ya Bajeti inayopendekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba tarehe 18 Februari, 2022 Serikali iliwasilisha Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya mwaka 2021/2022, nyongeza iliyojulikana kwa jina maarufu la Fedha za UVIKO.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Bunge hili watakuwa mashahidi wa namna nyongeza ile ilivyoleta mafanikio makubwa katika sekta za afya, elimu, maji na utalii. Hakika sote tutakuwa mashahidi kwa umma na historia itatukumbuka kwa uamuzi makini, thabiti na wenye mwelekeo wa kimaendeleo katika Taifa letu la Tanzania kwa uamuzi tulioufanya mwaka 2022 na ambao tunaenda kuufanya leo, tarehe 14 Februari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake binafsi katika kuliletea Taifa maendeleo. Haya ninayoyasema yanathibitishwa na masuala yafuatayo ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa kinara: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba mazingira ndio kihatarishi kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi. Mheshimiwa Rais ameliona hilo na ameanza kwa kujikita kwenye nishati safi ya kupikia. Ni kutokana na jitihada hizo tulishuhudia Mkutano mkubwa wa Nishati Afrika uliofanyika Tanzania na kuhudhuriwa na Marais 21 kutoka nchi mbalimbali za Afrika: -

(i) Sekta ya utalii imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza nakisi ya urari wa jumla wa malipo na huduma kutoka dola milioni 807.8 mwaka 2023 hadi dola milioni 364.2 mwaka 2024. Nani anaweza kupinga hizi sio juhudi za

Mheshimiwa Rais baada ya filamu yake ya *The Royal Tour;*

(ii) Tarehe 4 Februari, 2025 Mheshimiwa Rais alipokea tuzo kutoka kwa Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia kutoka Taasisi ya *The Gates.* Pamoja na sababu nyingine, Mheshimiwa Rais ametunukiwa tuzo hiyo kutokana na juhudi zake katika mapambano dhidi ya vifo vya akinamama wajawazito na watoto wachanga chini ya umri wa miaka mitano; na

(iii) Amani, utulivu na mshikamano ndio nguzo kuu ya maendeleo ya Taifa lolote duniani. Kulithibitisha hilo, tarehe 8 Februari, 2025, Mheshimiwa Rais alipokea Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* kwa lengo la kutafuta suluhu ya mgogoro wa Kongo Mashariki na hapa nyumbani ameendelea kutekeleza falsafa yake ya *4R* yaani *(Reconciliation, Resilience, Reform and Rebuilding)*. Huyu ndiye Rais Watanzania tunayemhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda hautoshi kuelezea mafanikio ya Mheshimiwa Rais kwa kipindi ambacho amekuwa madarakani hadi hivi sasa. Itoshe tu kusema anastahili kuendelea kuliongoza Taifa hili na tutarajie mengi mazuri zaidi chini ya uongozi wake. Kamwe, Kamati ya Bajeti haitakuwa kikwazo katika kufanikisha sera za kiuchumi na kibajeti za Mheshimiwa Rais, bali kumshauri kupitia Bunge lako namna bora ya kuziboresha, ili ziwe na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la fedha za nyongeza ya bajeti; Dirisha la Ustahimilivu na Uendelevu (*The Resilience and Sustainability Facility-RSF)* hutoa ufadhili wa muda mrefu na kwa riba nafuu kwa nchi zinazofanya mageuzi, ili kupunguza athari zinazoathiri nakisi ya urari wa malipo ya ujumla *(overall balance of payment deficit)* yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Pamoja na masharti mengine, ili nchi iweze kupata fedha kutoka dirisha hili, ni lazima iwe imeonesha masuala makuu mawili:-

(i) Mabadiliko ya kisera ya hali ya juu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na maandalizi ya kujilinda dhidi ya athari za majanga; na

(ii) Uhimilivu wa deni na uwezo wa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo hivi vimeiwezesha Tanzania kupata jumla ya dola milioni 55.9, sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 142.69. Waswahili husema, ukiona vyaelea ujue vimeundwa. Huu ni ushahidi mwingine wa uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakika Mheshimiwa Rais anastahili miaka mitano tena ili aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi tuliyoyachukua Wajumbe wa Mkutano Mkuu yalikuwa ni sahihi, kwa wakati sahihi na kwa mtu sahihi. Nani kama Dkt. Samia?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* na Benki ya Maendeleo ya Africa *(AfDB);* Serikali imepokea mikopo miwili kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* dola za Marekani milioni 191.33 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 486 na dola za Marekani milioni 181.32 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 460 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB)*. Mikopo hii pamoja na kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ina lengo la kupunguza madeni ya wakandarasi waliotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba fedha hizi hazikuwa sehemu ya bajeti, ilikuwa ni lazima Serikali kuwasilisha nyongeza ya bajeti Bungeni ili ipate ridhaa ya kutumia fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya kisheria na kikatiba kuhusu uwasilishaji wa mapendekezo ya nyongeza ya bajeti ya mwaka 2024/2025 *(Supplementary Budget);* Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka misingi na mazingira ambapo Serikali inaweza kuleta *supplementary budget*. Ibara ya 137(3), inasema ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba:-

(i) Fedha za matumizi zilizoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, kwa ajili ya shughuli fulani hazitoshi au kwamba imekuwa lazima kulipa gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria; au

(ii) Kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli fulani kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi yaliyoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo au kwamba fedha zimetumiwa kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara hiyo inasisitiza Serikali kuwasilisha Bungeni makadirio ya matumizi ya nyongeza au kadiri itakavyokuwa au maelezo ya matumizi ya ziada. Baada ya Bunge kuyakubali mapendekezo hayo ya makadirio ya matumizi ya nyongeza au maelezo ya matumizi ya ziada utawasilishwa Bungeni, Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika na hayo makadirio au maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439; kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kinafafanua zaidi Ibara ya 137(3) ya Katiba kwa kuweka mazingatio na utaratibu wa uwasilishaji wa *supplementary budget* Bungeni. Aidha, kifungu kidogo cha (3) kinaelekeza kwamba mara baada ya Serikali kuwasilisha *supplementary budget* Bungeni itaambatana na Muswada wa Sheria ya Matumizi ili uidhinishwe na Bunge. Hivyo, bajeti hii inayowasilishwa Bungeni ni utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Bajeti kutokana na upatikanaji wa jumla ya dola za Marekani 372,653,704.65 sawa na shilingi za Kitanzania 945,720,571,662.77.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2205; Kamati ilipitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka, Julai hadi Disemba, 2024/2025 na ilibaini kuwa Serikali ilipokea fedha kutoka *AfDB* na *IMF* ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa

na Bunge. Fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* shilingi bilioni 460 zilikuwa zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024, lakini zikachelewa kupokelewa kwa wakati. Aidha, fedha za *IMF* jumla ya shilingi bilioni 486, majadiliano yalikamilika katika kipindi ambacho Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali yalishawasilishwa na kuidhinishwa na Bunge. Hivyo, kulikuwa na umuhimu wa kufanya marejeo ya makusanyo, pamoja na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa sababu ya upatikanaji wa fedha kutoka *IMF* na *AfDB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo zinatarajiwa kutumika kutekeleza shughuli ambazo hazikuwa zimepangwa kwenye bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge, pamoja na kuongeza fedha zaidi ya zile zilizokuwa zimepangwa kwa baadhi ya shughuli ambapo zilikuwa kwenye bajeti na ziliidhinishwa na Bunge na haziwezi kutekelezwa kupitia uhamisho. Kwa mujibu wa Katiba na Sheria, Serikali isingeweza kufanya matumizi bila kuleta maombi kwa Bunge, ili liidhinishe nyongeza na kupata ridhaa ya matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za mkopo; majadiliano baina ya Kamati ya Bajeti na Serikali; utakumbuka kwamba ofisi yako iliridhia Kamati ya Bunge ya Bajeti ikutane na Serikali tarehe 5, 6 na 7 Februari, 2025, kwa ajili ya kujadili Mapendekezo ya Mpango na Mgawanyo wa Fedha zenye jumla ya shilingi bilioni 945.7. Kikao hicho kilifanyika kama ulivyoelekeza na kilikuwa baina ya Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa mgawanyo wa fedha hizo kwa kuangalia randama za mafungu yaliyoguswa na ongezeko hilo, shughuli zinazoenda kutekelezwa, sababu za Serikali kutenga kiasi hicho na mahitaji ya fedha kwa sasa. Kimsingi Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu mgao wa Fungu 21 – Hazina na Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na haikukubaliana na matumizi yaliyokuwa yamependekezwa na Serikali kwa Fungu 52 – Wizara ya Afya, Fungu 056 – Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano na mashauriano ya kina baina ya Kamati na Serikali, masuala yafuatayo yalikubalika:-

(i) Kuhamisha shilingi bilioni 70 kutoka Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii na kuzipeleka Fungu 56 – Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya maboma ya shule, madarasa, zahanati na vituo vya afya yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi na si kuanzisha majengo mapya;

(ii) Kuhamisha shilingi bilioni 53.5 kutoka Fungu 52 – Wizara ya Afya kwenda Fungu 56 – Ofisi ya Rais-TAMISEMI ili zikajenge vituo vya afya vipya 214 katika kila Jimbo la Tanzania Bara kwa wastani wa gharama za ujenzi za shilingi milioni 250 kwa kituo; na

(iii) Kuhamisha shilingi bilioni 30 kutoka Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda Fungu 56 – Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili ziongeze fedha zitakazoelekezwa *TARURA* kutoka shilingi bilioni 20 hadi shilingi bilioni 50, kwa ajili ya kujenga madaraja maeneo korofi na kurejesha mawasiliano sehemu ambazo yamekatika kutokana na mvua zinazoendelea. Hii ndiyo kazi inayoifanya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bajeti naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuonesha utayari wake wa kukubali mapendekezo ya Kamati. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha ambaye hakusita kuyapokea mapendekezo ya Kamati na kuyafikisha kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya maamuzi. Huyu ndiye Rais ambaye Watanzania tunakwenda kumpigia kura mwaka 2025. Mgawanyo wa fedha ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa ujumla kuhusu mgawanyo wa fedha; ukirejea Jedwali Namba 1 kama linavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati utaona kwamba

38.32% ya fedha zote zimeelekezwa kwenye matumizi ya kawaida na 61.68% ni, kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi 38.32% zinaenda kulipia miradi ya maendeleo ambayo imekwisha kutekelezwa na wakandarasi wanaidai Serikali fedha na si kwamba zote zinaenda kutumika katika shughuli za uendeshaji. Mfano mzuri ni Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* ilinunua mitambo kwa ajili ya ukarabati wa barabara. Hata hivyo, mitambo hiyo haifanyi kazi kwa sababu hakuna fedha kwa ajili ya kuiendesha. Hivyo, ieleweke kwamba fedha hizi zinaonekana ni za matumizi ya kawaida, ila kwa uasili zinaenda kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo ya jumla; Kamati ina ushauri wa ujumla kuhusu matumizi ya fedha hizo kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kimkakati kila Jimbo

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ilikwishachukua orodha ya vituo vya afya vya kimkakati vinavyotakiwa kujengwa kila jimbo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, basi orodha ile iheshimiwe na ndio itumike katika ujenzi. Kumekuwa na kasumba kwa baadhi ya watendaji, pindi fedha zinapopelekwa katika Halmashauri kufanya maamuzi tofauti na mapendekezo ambayo yanakuwa yamepitishwa na Bunge, Kamati ya Bajeti katika Bunge la mwezi Machi, 2025 itafanya ufuatiliaji wa utolewaji wa fedha na ujenzi wa vituo hivyo vya afya na endapo itaonekana orodha imekiukwa itapendekeza kwa Bunge hatua stahiki za kuchukua kwa wahusika. *(Makofi)*

(ii) Ukamilishaji wa maboma yalioanzishwa kwa nguvu za wananchi

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mwaka 2024 ilikamilisha tathmini ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma yote nchini na kubaini kwamba zilihitajika shilingi bilioni 228.24. Hivyo, kiwango kinachopendekezwa cha shilingi bilioni 71 kitapunguza mzigo wa ujenzi wa maboma kwa walau 31.1%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa rai kwa Serikali kwamba mgawanyo wa fedha hizi uzingatie mahitaji, hali ya uchumi ya halmashauri, uwezo wa kimapato na mgawanyo linganifu. Kamati haitarajii kuona kuna majimbo yananufaika kuliko mengine bila kuzingatia viashiria hivyo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha orodha ya maboma yatakayokamilishwa mapema iwezekanavyo ili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kuyahakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya fedha zilizopatikana kupitia nyongeza hii ya bajeti; uzoefu unaonesha zinapopatikana fedha na mwaka wa fedha unaenda kwisha, masuala mawili hujitokeza, ama kuwe na matumizi mabaya au fedha zirudishwe Hazina kutokana na fungu husika kushindwa kutumia hadi mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa wakati *(Real Time Audit)* ya fedha hizi ili kuzuia ubadhirifu na inatoa rai kwa Maafisa Masuuli wote kufuata Kanuni na Sheria ya Bajeti, Sura Namba 439 ambazo zinawataka kumjulisha Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu fedha za maendeleo ambazo wanaomba kuvuka nazo mwaka siku 30 kabla ya tarehe ya mwisho ya kutekeleza bajeti ya mwaka husika ili wazitumie katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi; Waswahili husema pongezi humtia mtu bidii. Kwa kifupi nieleze kwa nini lazima kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pongezi hizi nazitoa kutokana na utayari wake wa kupokea maoni ya Kamati, kuyakubali na kuyazingatia katika ongezeko hili la bajeti. Huyu ndiye Rais ambaye Watanzania tunamhitaji, mwenye uwezo wa kuchukua maoni, kuyafanyia kazi, kutoa maamuzi kwa maslahi mapana ya Watanzania. Nani kama Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; ninaomba nihitimishe kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika - Dkt. Tulia Ackson, Mbunge kwa kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii. Vilevile nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika na naomba

vilevile nimpongeze Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Naibu Waziri wa Fedha – Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba - Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Ndugu Meshack Anyingisye - Kamishna wa Bajeti na Ndugu Johnson Nyella - Kamishna wa Sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti chini ya uongozi thabiti na mahiri wa baba yangu, mlezi wangu na Mwenyekiti Mheshimiwa Oran Manase Njeza, naamini wajumbe na wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini watamrudisha Bungeni kwa kishindo baba huyu kwa sababu amekuwa hazina kwa Taifa hili na katika kuweza kuendesha Kamati yetu ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba niwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inaisimamia Serikali ipasavyo. Majina ya Wajumbe hao ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Ndugu Baraka Leonard - Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili na hatimaye kupitisha Mapendekezo ya Serikali ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**14 FEBRUARI, 2025**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2024/25 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Nyongeza ya Bajeti inayopendekezwa na Serikali. Utakumbuka kwamba tarehe 18 Februari, 2022, Serikali iliwasilisha mapendekezo ya nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/22, nyongeza iliyojulikana kwa jina maarufu *"Fedha za Uviko"*. Wabunge wa Bunge hili watakuwa mashahidi wa namna nyongeza ile ilivyoleta mafanikio makubwa katika sekta za afya, elimu, maji na utalii. Hakika sote tutakuwa mashahidi kwa umma na historia itatukumbuka kwa uamuzi makini, thabiti na wenye mwelekeo wa kimaendeleo katika Taifa letu la Tanzania kwa uamuzi tulioufanya mwaka 2022 na ambao tunaenda kuufanya leo tarehe 14 Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, *"Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo"*. Naomba nimpongeze **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa Juhudi zake binafsi katika kuliletea Taifa maendeleo. Haya ninayoyasema yanathibitishwa na masuala yafuatayo ambayo Mhe. Rais amekuwa kinara:-

i. Sote tunatambua kwamba mazingira ndio kihatarishi kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi. Mhe. Rais ameliona hilo na ameanza kwa kujikita kwenye nishati safi ya kupikia. Ni kutokana na jitihada hizo tulishuhudia Mkutano mkubwa wa Nishati Afrika uliofanyika Tanzania na kuhudhuriwa na Marais 21 kutoka nchi mbalimbali za Afrika;

ii. Sekta ya utalii imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza nakisi ya Urari wa Jumla wa Malipo na Huduma kutoka **Dola za milioni 807.8** mwaka 2023 hadi **Dola za milioni 364.2** mwaka 2024.

Nani anaweza kupinga hizi sio juhudi za Mhe. Rais baada ya Filamu yake ya *The Royal Tour*;

iii. Tarehe 04 Februari, 2025 Mhe. Rais alipokea Tuzo kutoka kwa Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia kutoka Taasisi ya *Gates*. Pamoja na sababu nyingine, Mhe. Rais ametunukiwa Tuzo hiyo kutokana na juhudi zake katika mapambano dhidi ya vifo vya kina mama wajawazito na watoto wachanga chini ya umri wa miaka mitano; na

iv. Amani, utulivu na mshikamano ndio nguzo kuu ya maendeleo ya Taifa lolote Dunia. Kulithibitisha hilo tarehe 08 Februari, 2025, Mhe. Rais alipokea Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa lengo la kutafuta suluhu ya mgogoro wa Kongo mashariki na hapa nyumbani ameendelea kutekeleza falsafa yake ya 4R yaani *(Reconciliation, Resilience, Reform and Rebuilding)*.

**Mheshimiwa Spika,** muda hautoshi kuelezea mafaniko ya Mhe. Rais kwa kipindi ambacho amekuwa madarakani hadi hivi sasa. Itoshe tu kusema anastahili kuendelea kuliongoza Taifa hili na tutarajie mengi mazuri zaidi chini ya uongozi wake. Kamwe Kamati ya Bajeti haitakuwa kikwazo katika kufanikisha Sera za Kiuchumi na Kibajeti za Mhe. Rais bali kumshauri kupitia Bunge lako namna bora ya kuziboresha ili ziwe na tija.

## 2.0. CHIMBUKO LA FEDHA ZA NYONGEZA YA BAJETI

### 2.1. Dirisha la Ustahimilivu na Uendelevu *(The Resilience and Sustainability Facility-RSF)*

**Mheshimiwa Spika,** Dirisha la Ustahimilivu na Uendelevu (RSF) hutoa ufadhili wa muda mrefu na kwa riba nafuu kwa nchi zinazofanya mageuzi ili kupunguza athari zinazoathiri nakisi ya urari wa malipo ya ujumla *(Overall Balance of Payment Deficit)* yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Pamoja na masharti mengine ili nchi iweze kupata fedha kutoka dirisha hili ni lazima iwe imeonyesha masuala makuu mawili:-

i. Mabadiliko ya kisera ya hali ya juu ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi na maandalizi ya kujilinda dhidi ya athari za majanga; na

ii. Uhimilivu wa deni na uwezo wa kulipa.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo hivi vimeiwezesha Tanzania kupata jumla ya **Dola milioni 55.9** sawa na **Shilingi za Kitanzania bilioni 142.69.** Waswahili husema *"ukiona vyaelea ujue vimeundwa"* huu ni ushahidi mwingine wa Uongozi thabiti wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, hakika Mhe. Rais anastahili miaka mitano tena ili aendelee kuwatumikia Watanzania.

## 2.2. Mikopo Kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB)

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepokea mikopo miwili kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) **Dola za milioni 191.33** sawa na **Shilingi za Kitanzania bilioni 486** na **Dola milioni 181.32** sawa na **Shilingi za Kitanzania bilioni 460** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mikopo hii pamoja na kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ina lengo la kupunguza madeni ya wakandarasi waliotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukweli kwamba fedha hizi hazikuwa sehemu ya Bajeti, ilikuwa ni lazima Serikali kuwasilisha Nyongeza ya Bajeti Bungeni ili ipate ridhaa ya kutumia fedha hizo.

## 3.0. MISINGI YA KISHERIA NA KIKATIBA KUHUSU UWASILISHAJI WA MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2024/25 *(SUPPLIMENTARY BUDGET)*

## 3.1. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

**Mheshimiwa Spika,** katiba ya nchi imeweka misingi na mazingira ambapo Serikali inaweza kuleta *supplementary budget*. Ibara ya 137 Ibara ndogo ya (3) inasema ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba:-

a) Fedha za matumizi zilizoidhinishwa na sheria ya matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya shughuli fulani hazitoshi au kwamba imekuwa lazima kulipa gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria; au

b) Kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli fulani kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi yaliyoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo au kwamba fedha zimetumiwa kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa Sheria.[1]

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hiyo inasisitiza Serikali kuwasilisha Bungeni makadirio ya matumizi ya nyongeza au, kadri itakavyokuwa, maelezo ya matumizi ya ziada. Baada ya Bunge kuyakubali mapendekezo hayo ya makadirio ya matumizi ya nyongeza au maelezo ya matumizi ya ziada, utawasilishwa Bungeni Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika na hayo makadirio au maelezo.

### 3.2. Sheria ya Bajeti Sura ya 439

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Kinafafanua zaidi Ibara ya 137(3) ya Katiba kwa kuweka mazingatio na utaratibu wa uwasilishaji wa *supplimentary budget* Bungeni. Aidha, kifungu kidogo cha 3 kinaelekeza kwamba mara baada ya Serikali kuwasilisha *supplimentary budget* Bungeni itaambatana na Muswada wa Sheria ya Matumizi ili uidhinishwe na Bunge. Hivyo, Bajeti hii inayowasilishwa Bungeni ni utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Bajeti kutokana na kupatikana kwa jumla ya **Dola za 372,653,704.65** sawa na **Shilingi za Kitanzania 945,720,571,662.77.**

[1] The Constitution of United Republic of Tanzania of 1977

### 3.3. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka Julai-Disemba 2024/25 na ilibaini kuwa Serikali ilipokea fedha kutoka AfDB na IMF ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) **Shilingi bilioni 460** zilikuwa zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2023/24 lakini zikachelewa kupokelewa kwa wakati. Aidha, fedha za IMF jumla ya **Shilingi bilioni 486** majadiliano yalikamilika katika kipindi ambacho mapendekezo ya bajeti ya Serikali yalishawasilishwa na kuidhinishwa na Bunge. Hivyo kulikuwa na umuhimu wa kufanya marejeo ya makusanyo pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/25 kwa sababu ya upatikanaji wa fedha kutoka IMF na AfDB.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha hizo zinatarajiwa kutumika kutekeleza shughuli ambazo hazikuwa zimepangwa kwenye Bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge pamoja na kuongeza fedha zaidi ya zile zilizokuwa zimepangwa kwa baadhi ya shughuli ambapo zilikuwa kwenye Bajeti na ziliidhinishwa na Bunge na haziwezi kutekelezwa kupitia uhamisho. Kwa mujibu wa Katiba na Sheria Serikali isingeweza kufanya matumizi bila kuleta maombi kwa Bunge ili liidhinishe nyongeza na kupata ridhaa ya matumizi.

## 4.0. MGAWANYO WA FEDHA ZA MKOPO

### 4.1. Majadiliano baina ya Kamati ya Bajeti na Serikali

**Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kwamba uliridhia Kamati ya Bunge ya Bajeti ikutane na Serikali tarehe 5, 6 na 7 Februari, 2025 kwa ajili ya kujadili mapendekezo ya Mpango na Mgawanyo wa Fedha zenye jumla ya **Shilingi bilioni 945.7.** Kikao hicho kilifanyika kama ulivyoelekeza na kilikuwa baina ya Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa mgawanyo wa fedha hizo kwa kuangalia randama za mafungu yaliyoguswa na ongezeko hilo, shughuli zinazoenda kutekelezwa, sababu za Serikali kutenga kiasi hicho na mahitaji ya fedha kwa

sasa. Kimsingi Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu mgao wa **Fungu 21** Hazina na **Fungu 46** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na haikukubaliana na matumizi yaliyokuwa yamependekezwa na Serikali kwa **Fungu 052** Wizara ya Afya, **Fungu 056** Ofisi ya Rais-TAMISEMI na **Fungu 069** Wizara ya Malisili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya majadiliano na mashauriano ya kina baina ya Kamati na Serikali masuala yafuatayo yalikubalika:-

i. Kuhamisha **Shilingi bilioni 70** kutoka **Fungu 069:** Wizara ya Maliasili na Utalii na kuzipeleka **Fungu 056:** Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya maboma ya Shule, Madarasa, Zahanati na Vituo vya Afya yalioanzishwa kwa nguvu za wananchi na si kuanzisha majengo mapya;

ii. Kuhamisha **Shilingi bilioni 53.5** kutoka **Fungu 052:** Wizara ya Afya kwenda **Fungu 056:** Ofisi ya Rais-TAMISEMI ili zikajenge vituo vya afya vipya **214** katika kila jimbo la Tanzania Bara kwa wastani wa gharama za ujenzi za **Shilingi milioni 250** kwa kituo; na

iii. Kuhamisha **Shilingi bilioni 30** kutoka **Fungu 069:** Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda **Fungu 056:** Ofisi ya Rais-TAMISEMI ili ziongeze fedha zitakazoelekezwa TARURA kutoka **Shilingi bilioni 20** hadi **Shilingi bilioni 50** kwa ajili ya kujenga madaraja maeneo korofi na kurejesha mawasiliano sehemu ambayo yamekatika kutokana na mvua zinazoendelea.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Bajeti naomba nimpongeze **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuonyesha utayari wake wa kukubali mapendekezo ya Kamati. Aidha, Kamati inampongeza **Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** Waziri wa Fedha ambaye hakusita kuyapokea mapendekezo ya Kamati na kuyafikisha kwa Mhe. Rais kwa ajili ya Maamuzi.

**Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa Nyongeza Baada ya Majadiliano**

| FUNGU NA. | MATUMIZI YA KAWAIDA | MATUMIZI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 021: Hazina | 175,801,747,090.20 | 150,168,072,344.96 | 325,969,819,435.16 |
| 046: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | | 131,441,381,625.19 | 131,441,381,625.19 |
| 052: Wizara ya Afya | | 53,771,474,301.22 | 53,771,474,301.215 |
| 056: Ofisi ya Rais - TAMISEMI | | 173,771,474,301.22 | 173,771,474,301.22 |
| 069: Wizara ya Maliasili na Utalii | 186,622,405,000.00 | 74,144,017,000.00 | 260,766,422,000.00 |
| **JUMLA** | **362,424,152,090.20** | **583,296,419,572.58** | **945,720,571,662.78** |

### 4.2. Ufafanuzi wa Ujumla kuhusu Mgawanyo wa Fedha

**Mheshimiwa Spika,** ukirejea jedwali na 1 utaona kwamba **asilimia 38.32** ya fedha zote zimelekezwa kwenye matumizi ya kawaida na **asilimia 61.68** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kimsingi **asilimia 38.32** zinaenda kulipia miradi ya maendeleo ambayo imekwisha kutekelezwa na wakandarasi wanaidai Serikali fedha na si kwamba zote zinaenda kutumika katika shughuli za uendeshaji. Mfano mzuri ni Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ilinunua mitambo kwa ajili ya ukarabati wa barabara hata hivyo mitambo hiyo haifanyi kazi kwa sababu hakuna fedha kwa ajili ya kuiendesha. Hivyo, ieleweke kwamba fedha hizi zinaonekana za matumizi ya kawaida ila kwa uasili zinaenda kutekeleza miradi ya maendeleo.

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina ushauri wa ujumla kuhusu matumizi ya fedha hizo kama ifuatavyo:-

### 5.1. Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kimkakati Kila Jimbo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali ilikwisha chukua orodha ya vituo vya afya vya kimkakati vinavyotakiwa kujengwa kila jimbo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, basi orodha ile iheshimiwe

na ndio itumike katika ujenzi. Kumekuwa na kasumba kwa baadhi watendaji pindi fedha zinapopelekwa katika Halmashauri kufanya maamuzi tofauti na mapendekezo ambayo yanakuwa yamepitishwa na Bunge. Kamati ya Bajeti katika Bunge la mwezi **Machi 2025**, itafanya ufuatiliaji wa utolewaji wa fedha na ujenzi wa vituo hivyo vya afya na endapo itaonekana orodha imekiukwa itapendekeza kwa Bunge hatua stahiki za kuchukua kwa wahusika.

### 5.2. Ukamilishaji wa Maboma yalioanzishwa kwa nguvu za Wananchi

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI mwaka 2024 ilikamilisha tathmini ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma yote nchini na kubaini kwamba zilihitajika **shilingi bilioni 228.24.** Hivyo, kiwango kinachopendekezwa cha **shilingi bilioni 71** kitapungunguza mzigo wa ujenzi wa maboma kwa walau **asilimia 31.1**. Kamati inatoa rai kwa Serikali kwamba mgawanyo wa fedha hizi uzingatie mahitaji, hali ya uchumi ya Halmashauri, uwezo wa kimapato na mgawanyo linganifu. Kamati haitarajii kuona kuna majimbo yananufaika kuliko mengine bila kuzingatia viashiria hivyo. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha orodha ya maboma yatakayokamilishwa mapema iwezekanavyo ili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kuyahakiki.

### 5.3. Matumizi ya Fedha zilizopatikana kupitia nyongeza hii ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** uzoefu unaonyesha zinapopatikana fedha na mwaka wa fedha unaenda kuisha masuala mawili hujitokeza ama kuwe na matumizi mabaya au fedha zirudishwe hazina kutokana na fungu husika kushindwa kutumia hadi mwisho wa Mwaka. Kamati inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya ukaguzi wa Wakati yaani *Real Time Audit* ya Fedha hizi ili kuzuia ubadhirifu na inatoa rai kwa maafisa masuuli wote kufuata kanuni za Sheria ya Bajeti Sura ya 439 ambazo zinawataka kumjulisha mlipaji mkuu wa Serikali kuhusu fedha za maendeleo ambazo wanaomba kuvuka nazo mwaka siku 30 kabla ya tarehe ya mwisho ya kutekeleza Bajeti ya mwaka husika ili wazitumie katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata.

## 6.0. PONGEZI

**Mheshimiwa Spika,** waswahili husema pongezi humtia mtu bidii, kwa kifupi nieleze kwa nini lazima kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.** Pongezi hizi nazitoa kutokana na utayari wake wa kupokea maoni ya Kamati, kuyakubali na kuyazingatia katika ongezeko hili la Bajeti.

## 7.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza kwanza wewe Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson, (Mb) kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, (Mb) Naibu Spika kwa kukusaidia vyema Mheshimiwa Spika. Aidha, napenda kumpongeza Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb) Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, (Mb) Naibu Waziri wa Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Ndg. Meshack Anyingisye, Kamishna wa Bajeti pamoja na Ndg. Johnson Nyella, Kamishna wa Sera.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inasimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Yahya Mhata, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Bw. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili na hatimaye kupitisha Mapendekezo ya Serikali ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2024/25.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Oran Njeza, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
14 Februari, 2025

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imetolewa na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine, kwanza, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe hongera kwa kusoma vizuri na nimeambiwa mwanao Sabrina Mpembenwe yupo juu hebu asimame, hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Ofisi ya Bunge

imeandaa Jarida la Bunge, Toleo la Tisa. Jarida hili linaeleza masuala mbalimbali ya Kibunge ikiwemo matukio yaliyojiri wakati wa Mkutano wa Bunge wa Kumi na Saba na baadhi ya matukio katika Mkutano huu wa Kumi na Nane. Jarida hilo lilishawekwa katika Tovuti ya Bunge na kwenye vishikwambi vyenu na mengine mtagawiwa.

Waheshimiwa Wabunge, jarida ni hili ambao tumepata *hard copy* ndiyo hii na wale ambao wako kwenye vishkwambi mtasoma ili muelewe kazi mlizozifanya wenyewe kwenye Bunge.

Ahsante sana, namwita Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na namuita Mwenyekiti anishikie mara moja.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nahodha tuendelee.

**MHE. SHAMSI V. NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kutoa mchango wangu kwa bajeti hii ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa busara sana wa kuunga mkono juhudi za wananchi za kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya Taifa lao. Uamuzi wa Serikali wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo ya muda mrefu ya vituo vya afya, shule, vyuo vya *VETA* ambavyo vipo kwa muda mrefu mimi nafikiri uamuzi huu ni uamuzi wa busara sana, hasa tukitilia maanani kwamba lengo lake ni kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka Hayati Baba wa Taifa alisisitiza sana umuhimu wa kujenga Taifa lenye moyo wa kujitolea na kujitegemea. Kwa hiyo, mimi nadhani jambo hili ni la maana sana kwa muktadha huo. Hata hivyo, jambo hili lazima lisimamiwe kwa umakini ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za wananchi ili kuhakikisha kwamba ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya vituo vya afya, shule na vyuo vya *VETA* unafanywa kwa ubora unaotakiwa unakamilika kwa wakati na napenda nipendekeze mambo matatu ya msingi.

Kwanza, ukamilishaji wa majengo haya lazima uratibiwe na Wizara ya Mipango na Uwekezaji ili kuhakikisha kwamba Serikali kwanza inatenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha maboma ambayo yameachwa kwa muda mrefu yanakamilishwa angalau kwa kipindi cha miaka mitatu mpaka minne, huo ni ushauri wangu wa kwanza. *(Makofi)*

Pili, iwapo wananchi watabuni utaratibu wa ujenzi kama huu walioufanya wa kutumia nguvu za wananchi na kujenga vituo vya afya na kujenga shule siku zijazo tunaomba jambo hili liratibiwe kikamilifu na Wizara ya Mipango. Wizara ya Mipango iweke vigezo, iweke masharti na iweke ramani ili majengo yote ya Tanzania nzima yawe majengo yanayofanana badala ya kila Wilaya kuwa na majengo ya aina yake, lakini pili ujenzi huo utawekewa bajeti kila mwaka. *(Makofi)*

Tatu, Wizara ya Mipango na Uwekezaji ihakikishe kwamba ujenzi wa miradi ya wananchi ya shule na vituo vya afya unazingatia matumizi bora ya ardhi. Nataka kusema nini hapa? Mimi nafikiri wakati umefika badala ya kujenga majengo ya chini yaliyotawanyika kwenye eneo kubwa umefika wakati majengo haya yajengwe kwa kutumia majengo ya ghorofa ili ardhi yetu itumike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaamini kwamba ukamilishaji wa majengo haya niliyoyataja, majengo ya vituo vya afya, majengo ya *VETA* na majengo ya shule, ujenzi wake unaweza kufanikiwa sana iwapo Wizara ya Mipango ingetekeleza ushauri wa Bunge wa kuwa na mamlaka maalumu ya udhibiti na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali jambo ambalo mpaka sasa halijatekelezwa. Kwa hiyo, naiomba tu Wizara na Serikali ihakikishe kama tunataka kuratibu shughuli hizi za maendeleo kwa ufanisi zaidi ni vizuri basi wakazingatia ushauri huu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. Nimuite sasa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben aweze kuchangia.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Bunge na kiongozi wetu, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nyongeza ya bajeti hii, tafsiri ya jambo hili ni moja tu, ni kwamba tunakwenda kutumia zaidi ya tulivyokuwa tumepanga na tafsiri ya hiyo ni kwamba tunakwenda kupeleka huduma zaidi kwa wananchi zaidi ya tulivyokuwa tumepanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linafanyika kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 137(3), lakini na Sheria yetu ya Bajeti kifungu cha 43. Kwa hiyo, asitokee mtu akaja akapotoshapotosha jambo hili kana kwamba halifanyiki kwa utaratibu, maana wapo watu wamezoea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawezekana kutokana na uhimilivu wa deni na uwezo wa kulipa wa nchi yetu, ndiyo maana tumeweza kupata fedha hizi kutoka *IMF* jumla bilioni 486, lakini kutoka *African Development Bank* jumla bilioni 460 ambayo ndiyo inafanya jumla hiyo ya karibu bilioni 945.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo makubwa yanayokwenda kufanyika ya kitaifa yako mawili; kwanza ni malipo kwa wakandarasi wetu ambao wametekeleza na wanaendelea kutekeleza miradi ikiwemo miradi ya nishati, miradi ya maji, miradi ya uchukuzi na usafirishaji na maeneo mengine ya kimkakati ambayo yote nchi nzima tunayafahamu, *specifically* kwa majimbo yetu kila Mbunge hapa mambo yafuatayo ambayo ninakwenda kuyataja yanayofanyika Handeni ndiyo hayo hayo yanakwenda kufanyika kwa kila Jimbo kupitia bajeti hii ambayo tutaipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mtu niliyepata fursa ya kuchangia niwashawishi na niwaombe Wabunge wenzangu tupitishe nyongeza hii ya bajeti ili tupeleke huduma zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kujenga vyuo vya *VETA* vyote karibu 60 ambavyo ujenzi ulikuwa unaendelea, pale Handeni Mjini tunakwenda kuendelea na ujenzi wa chuo chetu

cha *VETA* kama tu ambavyo kule Lupembe kwa ndugu yangu Mheshimiwa Swalle hapa kwenye chuo chake pale Matiganjora naye ujenzi unaenda kuendelea, yupo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tupitisheni hii ili wananchi wa Lupembe kule Matiganjora wakashangilie chuo chao cha *VETA* kiendelee. Tunajenga chuo hicho cha *VETA* pale Handeni Mjini kama ambavyo Chuo cha Sikonge kule kwa Mheshimiwa Kakunda ambacho kipo Ipole na vyuo vyote vya *VETA* ambavyo vipo kwa kila Mheshimiwa Mbunge zaidi ya vyuo 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nyongeza hii ya bajeti inapeleka vifaatiba pamoja na dawa kwenye hospitali zetu zote kuanzia Hospitali za Rufaa, Hospitali za Kitaifa, Hospitali za Kimkoa, Hospitali za Kanda na Hospitali za Wilaya. Vivyo hivyo na kwenye vituo vya afya pamoja na zahanati. Kwa pale Handeni vituo vyetu vya afya vya Kideleko, Kituo cha Afya Kwedinguzu, Malezi pamoja na zahanati zetu za Hedi, Kwaruara, Kwasindi, Mankinda, Komnazi, Msasa, Kwedizando pamoja na Mkwajuni Shenika vyote vinakwenda kupata dawa na vifaatiba kupitia nyongeza ya bajeti hii tunayokwenda kuipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nyongeza hii aliyoileta hapa na ambayo sisi Wabunge leo tutakwenda kuipitisha, lakini vilevile kupitia nyongeza hii wananchi wa Kata ya Mabanda tunakwenda kupata kituo kipya cha afya.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Kakunda.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa msemaji kwamba hizi fedha zinakwenda mpaka kujenga Kituo cha Afya cha Kiloleli katika Wilaya ya Sikonge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa unaipokea hiyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hii na nimsisitize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeruhusu Wabunge wote hapa watoe taarifa kila mtu angetaja kituo cha afya ambacho kinakwenda kupata huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si tu hivyo, nyongeza hii ya bajeti inakwenda kutengeneza barabara zetu zote ambazo zilipata hitilafu kutokana na mvua nyingi zilizonyesha, ndiyo maana ni bajeti ya nyongeza ya kuungwa mkono, kule Handeni Mjini nyongeza hii inakwenda kutusaidia kutengeneza Barabara ya Misima – Nzeri, lakini vilevile na Malezi - Masampata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi hizi ambazo nimezitaja niungane na Wana-CCM wenzangu na niwapongeze sana Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa kwa kupiga kura zote za ndiyo na kutuletea Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Mwenyekiti wetu wa Chama kuwa mgombea pekee. Niwaambie Watanzania ni kazi sana kushindanisha kazi na maneno matupu, watapata taabu sana. Uchaguzi huu tunaokwenda kufanya mwaka huu ni uchaguzi tunaoshindanisha kazi na maneno matupu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni Watanzania tumchague Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura nyingi na Tanga tumejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimuite sasa Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami nianze kwa kusema kwamba kusema kweli

utaratibu huu wa *Supplementary Budget* ni utaratibu unaoonesha jinsi ambavyo Serikali inajali, Serikali ilivyosikivu na kujali uhimilivu wa utulivu wa uchumi wetu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Serikali ingeweza ikaja na mapato makubwa tu ikasema tutakopa bila kujua kama wataweza kukopa kutoka kwenye vyanzo ambavyo ni vya masharti nafuu, lakini Serikali iliona isiingize fedha hizi kwenye bajeti kabla ya kuwa na uhakika kwamba wataweza kuzipata kwenye vyanzo hivi ambavyo ni vya masharti nafuu ambavyo ni *IMF* na *African Development Bank. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kama wangeingiza tu mwanzoni bila kujua, Serikali nyingi zinaingia kwenye matatizo, wanayumbisha uchumi, wanalazimika kukopa fedha nyingi kutoka vyanzo ambavyo siyo himilivu na hivyo wanapoteza uhimilivu wa madeni yake. Kwa hiyo, mimi nasema huu mchakato ni mzuri na nampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu na mpendwa wetu na mgombea wa Urais kwa Kiti cha CCM mwaka huu 2025 naamini na wote tunajua kwamba tutampa kura zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nyongeza inaenda kutatua kero nyingi ambazo tulikuwa tunasikia hapa, tunaleta maswali yanakuja na naamini kwamba Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Afya, Waziri wa Elimu, hata Waziri wa Fedha mwenyewe alikuwa anajibu maswali hapa na sisi tunajiuliza anaposema kwamba tunapata kituo cha afya, lakini tukienda kwenye *line items* kwenye bajeti tuliyopitisha huoni. Anasema kwamba nitalipa makandarasi ambao sasa miradi mingi imesimama, unaenda kwenye bajeti tunaangalia kwenye bajeti tunasema mbona hatuoni hizo fedha? Tukawa tunasema hii Serikali inadanganya au inasemaje? Sasa wameleta hii nyongeza na inaenda kutatua matatizo yale ambayo tulifikiri kwamba wanadanganya kumbe walikuwa ni wasikivu walikuwa wanajua mchakato wa kuweza kupata fedha ambazo hazitayumbisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwa kweli ni kwamba kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alikuwa anatuambia kwamba mtapata vituo vya afya vile ambavyo mlikuwa

mmeomba kila Jimbo kituo kimoja. Tukawa tunalilia hapa tunasema tutakosa kura kule, lakini sasa tunaona kwamba milioni 250 zinaenda kwenye kila jimbo mara moja baada ya kupitisha bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini sasa anaweza akaenda kule kwenye jimbo langu ambako tulikuwa tumeainisha kujenga kituo hicho, naweza nikaenda nikasema jamani sasa tunarudi tena. Tulikuwa tunajiuliza haya masuala ya maboma ambayo yako mengi kwa kila jimbo na nashukuru kwamba Kamati ya Bajeti imeshaweka mwongozo wa namna gani tunatarajia kwamba Serikali itaenda kuainisha maboma yapi yatashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kuna maboma kwenye zahanati kama Kimangala kuna zahanati kama Wona, kule Kisimani ambazo ni maboma tu. Yapo pia madarasa mengi ambayo hayajakamilika naamini kwamba Serikali itaenda kuangalia namna gani ya kuainisha ni yapi ili na sisi tuweze kujumuishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha msingi zaidi ni kwamba Hazina imapata fedha ya ziada shilingi bilioni 325 ambapo wanaweza wakalipa wale wakandarasi ambao wanalia, ni wafanyabiashara wetu, benki zinapata matatizo, ukwasi umekuwa mzito kwenye benki kwa sababu wakandarasi walikuwa hawajalipwa. Shilingi bilioni 325 ni fedha nzuri na naamini wakishaenda kuzilipa hizo basi tutaanza kuona uchumi ukiendelea kutupa neema na kufurahisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaamini kwamba hivyo ni vitu vizito, kulipa madeni haya na vyote hivi pamoja na hivi vifaatiba ninaamini kwamba vinaenda kutupunguzia matatizo hasa katika kipindi hiki ambacho tunaenda kukamilisha awamu yetu ya Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninataka niseme kwamba tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu na tumpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake; Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na Gavana wa Benki Kuu kwa

sababu ninaamini kwamba wanaingia kwenye mchakato mzima huu wa kumshauri Mheshimiwa Rais namna ambavyo tunaweza tukaendeleza uchumi wetu ukaendelea kuwa himilivu, uwe na utulivu na *inflation* ikabaki chini, kwa sababu kama unavyoona kwamba hatuwezi kukopa fedha hovyo hovyo kwenye vyanzo vya ndani ambavyo vinaweza vikaongeza ukwasi kwa kazi ambayo hatujatarajia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** .... na hivyo kupunguza utulivu. Ninataka niseme, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuungane kwa pamoja tuipitishe nyongeza hii ya bajeti ili tukakamilishe hivyo vitu ambavyo nimevisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Charles Kimei. Sasa namwita Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa maono yake na mpaka kufanikisha jambo hili ambalo ni kubwa sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa usikivu wake, alitoa ushirikiano wa kutosha sana wakati tunafanya majadiliano ndani ya Kamati yetu na amekuwa *very accommodative,* ameelewa hisia za Wabunge na haya majibu ambayo yamekuwa yakitafutwa naamini tukisimamia vizuri tunaenda kupata matunda mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama katika mapendekezo ambayo tumekubaliana, katika Fungu 21 inaoneshwa kwamba kuna fedha zinakwenda kwenye matumizi ya kawaida. Kwa mtu ambaye hakupata nafasi ya kuchambua anaweza akadhani labda ni kwa ajili ya kwenda kulipana posho na kunywa chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba pale ambapo umekopa ukaenda kufanya miradi ya maendeleo, unapolazimika kwenda kulipa shughuli za maendeleo ambazo tayari wakandarasi wamekwishakufanya kazi ninadhani fedha hizi ni vizuri tukatafuta *formula,* isionekana kwamba ni matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matumizi ambayo yanakwenda kwenye shughuli za maendeleo kwa ajili ya kulipa wakandarasi wetu ambao tayari wamekwishafanya kazi za maendeleo. Kwa hiyo, ni vizuri wataalamu waendelee kuchakata hili ili isije ikaonekena kwamba ni matumizi ya kawaida. Kuwe na ufafanuzi ambao unaonesha matumizi haya ya kawaida ni kwa ajili ya shughuli gani na kimsingi ni shughuli za maendeleo ambazo zimefanyika katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwaomba wataalamu kwamba waendelee kuchakata ili kuona namna nzuri ambapo fedha zinapopatikana hata kama ni za mkopo, pale ambapo zinakwenda kufanya shughuli za maendeleo ni vizuri kwa mfanyabiashara yeyote ambaye urari unaonesha kwamba uko vizuri hata akienda kutafuta mkopo benki huwa anafikiriwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ambacho nakusudia kusema nini hapa? Kuna shughuli ambazo sisi kama Taifa tumefanya, ambazo ni kubwa, zinatakiwa zitupe mizania ambazo inasomeka vizuri. Kwa mfano tumekwenda kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere; katika hali ya kawaida kama ingekuwa ni mfanyabiashara ambaye anaonesha mizania yake ile ni *assert* ambayo inatakiwa ionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Taifa kwa uwekezaji mkubwa ambao tumefanya katika ujenzi wa Bwawa la Mwalimu

Nyerere tunapata wapi nafuu pale ambapo tunakwenda ku-*bargain* kutaka kukopa ili waone tayari sisi kama Taifa ni Taifa ambalo tunajiweza kwa sababu tuna uwekezaji mkubwa ambao umefanyika kiasi kwamba hata suala la kulipa siyo tatizo kwetu. Hii ni kwa sababu hatukukopa fedha tukaenda kulipana *allowance,* tumekopa fedha kwenda kuwekeza. Uwekezaji ambao unakuwa na tija kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida sitarajii na ni vizuri na *TIC* muanze kufikiria kwa namna nyingine, leo Tanzania tukisema tunatoa vivutio vya kikodi ndipo mtu aje kuwekeza, siyo sahihi. Miundombinu ambayo tumewekeza kama Taifa, kuwa na umeme wa kutosha inatakiwa iwe ni kivutio cha kutosha. Kwa hiyo, tuondokane na habari ya kutoa vivutio vya kikodi kwa sababu fedha hizi ambazo tumewekeza zinatakiwa zikafanye shughuli nyingine za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, ingekuwa ni mfanyabiashara hata ujenzi wa hii reli yetu ambayo hakika ni ufumbuzi mkubwa, Serikali ituoneshe katika *stock* walizo nazo uwekezaji huu tunauona wapi ili tunapokwenda kusema tunataka kukopa tuseme tuna *asset* kubwa ambayo kama Taifa tumewekeza fedha huko, ili tupate mkopo wenye masharti nafuu. Kwa sababu kama kuna nchi imeenda, imekopa, wakaenda kuishia kugawana posho lazima kuwe na tofauti na nchi kama Tanzania ambayo tunakopa na tunaenda kuwekeza katika miradi ambayo inazalisha na inaleta ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri wataalamu ndani ya Serikali muendelee kuchakata namna nzuri ya kuendelea kuripoti hesabu zetu, ili kama Taifa tukilinganishwa na mataifa mengine ioneshe jinsi ambavyo tumewekeza vizuri. Hatukukopa kwenda kugawana kama wengine ambavyo wanafanya. Kwa hiyo tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri wa Fedha na wataalamu kwa jinsi ambavyo wameweza kufanya mkopo huu ukaenda kutumika katika shughuli za maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge sote humu ni mashuhuda, ukienda Kalambo Kituo chetu cha Afya cha Kimkakati cha Katete sasa kitapata fedha. Nimwombe

Mheshimiwa Waziri, tumekubaliana kwamba fedha hizi zitoke mara moja ili ukifika mwezi wa tatu tukikutana panapo majaaliwa kila Mbunge atoe taarifa kwamba pesa zimekwishafika na zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna maboma mengi sana ambayo wananchi wametoa nguvu zao. Maboma hayo ni ya zahanati, shule za msingi na sekondari na mabwalo. Ni vizuri Serikali wakawashirikisha Wabunge pamoja na wataalamu ambao wanawatumia. Wabunge hawa ni sawa na mtu ambaye anavaa kiatu, ndiye anayejua ni wapi kinambana. Ni vizuri wakawashirikisha Wabunge ili kila mmoja atoe uhalisia kule anakotoka na fedha hizi zikafanye kazi iliyokusudiwa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Kandege. Sasa namwita Mheshimiwa Leah Komanya ilia atoe mchango wake.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ninaomba niunge mkono hoja iliyopo mbele yetu, pia na maoni ya Kamati ambayo mimi ni mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Kamati kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kukubali mapendekezo ya Kamati na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake mazuri. Pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa bega kwa bega na Kamati kwa ajili ya kuweza kupokea ushauri wetu. Mheshimiwa Rais amekubali mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhamisha shilingi bilioni 71 kutoka Maliasili na kupeleka TAMISEMI Fungu Namba 056 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma yaliyoanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tutakubali kwamba Serikali ilileta gharama ya shilingi bilioni 228 na ilielekeza maboma haya yatekelezwe na halmashauri zetu na sisi tunafahamu kwamba halmashauri zetu hazina uwezo wa kifedha kwa ajili ya kutekeleza maboma haya. Kwa hiyo, kwa kutoa shilingi bilioni 71 tukakuwa tumepunguza pale kwenye shilingi bilioni 228.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakubaliana na maoni ya Kamati kuwa Serikali iwashirikishe pia Wabunge kwa sababu tunayafahamu vizuri maboma haya. Mathalani katika Jimbo la Meatu hatuna maboma katika sekondari. Mahitaji makubwa yako katika shule za msingi ambapo tuna vyumba 90 vinahitaji kukamilishwa. Shule za msingi bado kuna msongamano wa watoto kukaa darasani pamoja na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiri kwamba kwa upande wa sekondari kupitia fedha za UVIKO Mheshimiwa Rais alifanya kazi kubwa sana ya kupunguza upungufu wa madarasa kiasi kwamba mpaka leo hii hakuna mwanafunzi anayesubiri madarasa yakamilishwe ili ajiunge na sekondari. Pia kuhamisha shilingi bilioni 30 kuzitoa Maliasili kwenda TAMISEMI, Fungu Namba 056 ili ziwe shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kujenga madaraja maeneo korofi. Wengi sana tunakiri kwamba *TARURA* ina changamoto ya fedha kwa sababu wakandarasi wengi wameondoka *site,* kwa hiyo, fedha hizi zitaenda kuwasaidia ili waweze kuendelea na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono uhamisho wa shilingi bilioni 53.5 kutoka Fungu Namba 052 - Afya kwenda TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa maboma. Hii imekuwa ni ahadi ya muda mrefu na sisi Wabunge tulikwenda kuwaaminisha wananchi wetu kwamba tutaleta maboma na vituo vya afya vya kimkakati. Jimbo la Meatu, Kata ya Ng'hoboko tutanufaika na ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga mkono kwenye lile jedwali letu ambapo shilingi bilioni 361 zimeelekezwa kwenye matumizi ya kawaida ambapo Fungu Namba 021 linaenda kupata shilingi bilioni 175.8 kwa ajili ya kwenda kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi. Tunajua kwamba

wakandarasi wetu wanadai. Mimi kama mjumbe ninashauri wakandarasi wa ndani wapewe kipaumbele ili kuwe na mzunguko wa fedha kwa wananchi wetu. Wengi tutakiri kwamba wakandarasi wengi wameondoka *site,* akiwepo mkandarasi aliyeko Jimbo la Meatu anayejenga Daraja la Itembe la shilingi bilioni 8.4 ambapo utekelezaji wa kazi amefanya kwa 85%, lakini malipo yako chini ya 30%. Hivyo anadai shilingi bilioni nne. Kwa hiyo, tukiwasaidia watarudi *site* na kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninashukuru kwa Fungu 046 Elimu kwa kupewa shilingi bilioni 131.4 kwa ajili ya kwenda kufanya utekelezaji. Sasa kipaumbele kitolewe kwenda *VETA* zilizoanzishwa ili ziweze kukamilika na ziweze kunufaisha watoto wetu kama ilivyokusudiwa ambapo watoto wengi wanakosa zile fursa zinazotoka Ofisi ya Waziri Mkuu....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** ... fursa zinazotoka Ofisi ya Waziri Mkuu na kwenda kusafiri mbali kutafuta *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu na Mheshimiwa Profesa Alexander Kitila ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naungana na Wabunge wengine wote waliochangia kuunga mkono jambo hili na ninawashawishi Wabunge wote tuunge mkono hoja hii ili ustawi wa wananchi wetu kule uweze kwenda kutekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kwenda kutafuta fedha hizi.

Ukiangalia jitihada za Serikali pia zinaonekana kule *TRA*. Si kwamba Serikali inaonekana tu inachukua hii mikopo yenye riba nafuu halafu mapato ya ndani hayakusanywi. Ukiangalia takwimu za *TRA* imeonesha kwamba nao wamekuwa wakiongeza sana ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, jambo hili ni jambo zuri na ni jambo la kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia halmashauri zetu nazo zinakusanya vizuri sana mapato kule. Hivi karibuni nilikuwa ninaangalia nikaona Halmashauri yangu ya Wilaya ya Ludewa tayari imeshavuka 70% na wanakwenda mbele. Jitihada zote hizi za kukusanya mapato ya ndani kupitia *TRA* na mapato ya halmashauri zetu na hii mikopo yenye masharti nafuu itaongeza sana ustawi wa wananchi wetu kule majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia hapa kwamba hata halmashauri yangu imevuka 70% na kwa hiyo ninawapongeza sana Mkurugenzi, Madiwani wote na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Olivanus Paul Thomas, anafanya kazi nzuri sana ya kusimamia mapato ya halmashauri. Kwa hiyo, fedha zile wanazokusanya *TRA* ambazo wanafanya Wakurugenzi kule na *non-tax revenue* zinavyoongezeka zikija kukusanyika na hizi ambazo ni mikopo yenye masharti nafuu tutaona mabadiliko kule majimboni kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaona kinachofanyika hapa ni jambo la utawala bora. Sisi Bunge tumepitisha sheria kwamba Wizara ya Fedha inapotaka kuongeza kitu chochote kwenye bajeti yake ya mwaka lazima warudi kwetu waanzie na Kamati ya Bunge ya Bajeti kisha walete Bungeni kwa ajili ya kuweza kuidhinisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bajeti yetu inavyoongezeka hayo ni mafanikio na ni jambo la kupongeza. Tukianza kuangalia tunaona kwamba fedha hizi zinakwenda kwenye ujenzi wa vyuo vya *VETA* nchini. Kwa hiyo, hata pale jimboni kwako Mkoani Njombe tumepewa Chuo cha *VETA* Shaurimoyo na kimeanza. Bado vitendea kazi vingine vilikuwa vinasubiriwa. Nina imani kupitia fedha hizi zitakwenda kuongeza

vitendea kazi kwenye Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Njombe ili kuinua taaluma ya mkoa ule na maeneo mengine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona kwamba kuna fedha zinakwenda Wizara ya Afya kwa ajili ya kununua vifaatiba, vitendanishi na dawa kwa ajili ya kutusaidia kule kwenye hospitali zetu za kanda, hasa hospitali za mikoa na kukarabati miundombinu kwenye hizi hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiangalia hata katika sekta ya afya Serikali yetu hii ya Awamu ya Sita imejitahidi kufanya mambo makubwa sana. Kuna vipimo vingi ambavyo wananchi walikuwa wanalazimika kuvifuata nje ya nchi, lakini sasa hivi ukienda kwenye hospitali ya kanda unavikuta. Kwa hiyo na fedha hizi zikienda huko zitakwenda kuboresha zaidi huduma ili wananchi wengi wasiende kutibiwa nje ya nchi kwa magonjwa ambayo yanaweza kutibika hapa hapa nchini. Kwa hiyo, itapunguza gharama za matibabu. Hiyo ndiyo sababu na mimi ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia zaidi unaona kwenye eneo la *TARURA* nao wanaenda kupata mgao wa fedha hizi. Sasa hivi tunazungumzia kukuza kilimo na kilimo bila barabara bora zile za vijijini ambazo zinatoka mashambani, itakuwa ni changamoto.

Kwa hiyo, ningependa niiombe Serikali ituhusishe sisi Wabunge kwa sababu tunajua. Mimi hata ukiniuliza jimboni kwangu kuna barabara zile chache ambazo zikifanyiwa ukarabati mkubwa tayari zinaunganisha jimbo zima. Mazao ya wakulima yanaweza kutoka shambani kwenda kwenye maeneo wanayohifadhi na kwenda masokoni kirahisi sana. Kwa mfano pale Mbwila na Lubonde wanalima sana vitunguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ile barabara inayoanzia Kigasi ikaenda Milo - Lundende mpaka Amani na maeneo mengine, hizi fedha zikipata tutapunguza changamoto za wananchi. Halikadhalika Kituo cha Afya Mawengi wananchi wamesubiri muda mrefu na kuna maboma mengi Jimboni Ludewa, Shule ya

Msingi Lubindi, Mangalanyene, wananchi wamefanya kazi kubwa kuna maboma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya hayo machache nitamke kwamba ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharius Kamonga. Sasa namwita Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Profesa Alexander Kitila ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika taarifa ambayo imewasilishwa hapa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutupa fursa hiyo na zawadi ya uhai na Bunge lako Tukufu kuandika tena historia. Nataka niseme kwamba historia inajirudia, kwa sababu ni Bunge hili hili la Kumi na Mbili, mwezi Februari, 2022 lilijadili na kuidhinisha nyongeza ya Bajeti ya mwaka 2021/2022 ya zaidi ya shilingi trilioni 1.3 ambapo shilingi trilioni moja ilikuwa ni kwa ajili ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tuliona kazi nzuri iliyofanyika kutokana na nyongeza ile ya bajeti hususani kwenye sekta ya afya ambapo zaidi ya shilingi bilioni 466 zilikwenda sekta ya afya, zikafanya kazi nzuri na matokeo tumeyaona ambapo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepata tuzo ya *Global Goalkeeper Award* iliyowasilishwa hivi karibuni kwa ajili ya kazi nzuri iliyowezesha kupungua kwa vifo vya akina mama na watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka 506 kwa vizazi hai 100,000 mpaka 104 kwa vizazi hai 100,000 ni kazi iliyotukuka na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ongezeko la shilingi bilioni 945 kwenye sekta zilezile ambazo nyingi zinategemewa na jamii, Sekta za Afya, Elimu, Maliasili na Miundombinu ni jambo la kuungwa

mkono. Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ambao karibu tutamaliza muda wetu, ninataka niishukuru Serikali kwa kulifanya Bunge hili kuwa Bunge ambalo linatimiza wajibu wake wa kuishauri na kuisimamia. Mara zote inapowasilisha kwenye Kamati yetu, kipindi chote hususan kwenye bajeti ya nyongeza imekuwa ikisikiliza maoni ya Kamati yanayotolewa kwa niaba ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa maoni haya ya kuidhinisha na kukubali kupeleka shilingi bilioni 71 kwa ajili ya maboma ambacho ni kilio. Tumeona jitihada za wananchi wa Tanzania wanaoiunga mkono Serikali yao kwa kuanzisha shughuli mbalimbali wakiamini mwenye nacho huongezwa. Kwa hiyo, Serikali inatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaipongeza kwa sababu ninatambua mkoa wetu wa Pwani una maboma mengi, hata Wilaya yetu ya Bagamoyo ina maboma mengi, Kata ya Zinga inaendelea na ujenzi wa shule shikizi, Kata ya Mapinga maeneo ya Kimele inajenga shule ya shikizi, Kata ya Nianjema na Kata ya Magomeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni imani yangu kwamba katika huo mgao basi halmashauri zetu zitakumbukwa. Kwenye hela zinazoenda kwenye elimu zaidi ya shilingi bilioni 131, tunaishukuru Serikali kwa kwenda kuanza ujenzi wa shule za sekondari za amali ambako Mkoa wa Pwani majimbo yote tisa tumepata hizo shule za sekondari na zimeanza ujenzi, ukiangalia kwenye Jimbo la Chalinze na Bagamoyo. Pia nina imani *VETA* inayojengwa kwenye Jimbo la Chalinze itakamilika kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, shilingi bilioni 50 inayokwenda *TARURA* tunatambua Serikali ina jitihada kubwa kuanzisha mfuko wa dharura kwa chanzo cha tozo kwenye matumizi ya mfuko wa reli ikaweka kwamba 50% itumike kwenye ukarabati wa miundombinu. Kwa hiyo, hii shilingi bilioni 50 inaenda kuongeza jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niiarifu Serikali, wapo pia wananchi wa maeneo mbalimbali wanatengeneza miundombinu yao kwa kujitolea. Kwa mfano, kwenye Kata ya Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo, Vitongoji vya Kibosha, Changohela na Kiharaka, wananchi wanatengeneza miundombinu ya barabara na Serikali ilituahidi. Kwa hiyo, nina imani katika shilingi bilioni 50 na maeneo mengine itakwenda kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatambua Wizara ya Maliasili imefikia lengo la watalii milioni tano. Ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutimiza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufikisha watalii milioni tano. Kwa hiyo, pesa zilizotengwa zitaenda kuhakikisha miundombinu inatengenezwa kwenye hifadhi zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya, ujenzi wa vituo vya afya vipya kwa kila jimbo inakwenda kuifanya Serikali yetu ivunje rekodi ya ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya kuliko wakati wowote. Kwa hiyo, ni jambo la kuishukuru Serikali imeona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, usione vyaelea vimeundwa, hii ndiyo maana sisi Wana-CCM wa Mkutano Mkuu tuliona Mheshimiwa Rais apewe kipindi cha pili kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kutafuta fedha za ziada ya kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo jambo rahisi, anaaminika kimataifa na diplomasia ya uchumi aliyoijenga imemfanya kuwa Rais ambaye ana ushawishi zaidi duniani. Matokeo yake ndiyo haya tunayaona. Bunge sasa lina meno ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Tumelifanya Bunge litembee kifua mbele kwamba katika uhai wake wa Bunge la Kumi na Mbili imeifanya Serikali itimize wajibu wake na kuvuka malengo ya utekelezaji wa ilani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchemba na Serikali nzima

na Wizara ya Fedha hongera kwa kazi nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu. Sasa ninamwita Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, wakati Profesa unakuja ngoja kidogo Mheshimiwa Naibu Spika anarejea kwenye Kiti.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mkumbo kabla hujaanza ninakuomba, wewe ni Waziri wa Uwekezaji, kuna taarifa ambazo zinapitapita kwenye mitandao zinaleta sintofahamu. Kwa vile wewe ni Waziri mwenye dhamana ya shughuli hiyo ninakuomba utoe kauli na uwaeleze Watanzania ukweli ulivyo, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa. Kuna mawili tu, kwanza ninaunga mkono hoja ambayo ipo mezani na miradi yote ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameieleza ni miradi muhimu katika mpango wetu wa maendeleo wa mwaka ambao tunautekeleza na nyingi zinakwenda kwenye kushughulikia miradi ya maendeleo ya wananchi na huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo umeniagiza nilifanye ni kutumia nafasi hii kutoa taarifa muhimu kuhusu yale ambayo yamejitokeza jana kwenye mitandao ya kijamii kuhusu uendelezaji wa Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo yaani *Bagamoyo Special Economic Zone*. Niseme mambo sita yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, Serikali ipo katika hatua mbalimbali za kutekeleza programu ya ujenzi wa Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo. Hii ni moja ya miradi 17 ya kielelezo iliyopo katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano 2021/2022, 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba pamoja na mambo mengine programu ya ujenzi wa eneo hili maalum la

kiuchumi la Bagamoyo inahusisha ujenzi wa miradi mingi. Moja ni ujenzi wa bandari, kongani za viwanda, kongani za TEHAMA, ukanda huru wa biashara na kituo cha reli. Kwa hiyo, siyo mradi mmoja ndiyo maana tunaita programu, ndani ya programu kuna miradi kadhaa pamoja na hiyo ambayo nimeitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, utekelezaji wa programu hii utafanywa na sekta binafsi kwa kushirikiana na Serikali kupitia mpango wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma yaani *Public Private Partnership (PPP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, wakati wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi wameonesha nia ya kuwekeza katika ujenzi wa miradi mbalimbali iliyoko katika programu hiyo, kwa kweli wadau wengi na wawekezaji wengi kutoka nchi mbalimbali wameonesha nia ya kushirikiana na Serikali katika kutekeleza programu hii na miradi mbalimbali ambayo ipo katika programu hiyo na kwa kweli wadau hawa wako katika hatua mbalimbali za mazungumzo na taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ni reli wanazungumza na reli, kama ni *port* wanazungumza na Mamlaka ya Bandari, kama ni viwanda wanazungumza na sisi Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara ya Viwanda na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tuhuma ambazo zinaendelea, Serikali haijaingia makubaliano au *commitment* yoyote na mwekezaji yeyote kwa sasa. Kwa hiyo, Serikali haina makubaliano yoyote wala hatuna mkataba na mwekezaji yeyote katika miradi ya Bagamoyo ambayo nimeitaja ukiwepo na mradi wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, taarifa zinazosambaa katika mitandao ya kijamii kwamba kampuni moja kutoka Saudi Arabia imepata mkataba wa uwekezaji wa kujenga na kuendesha Bandari ya Bagamoyo si za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie hiyo; kwa maelezo ambayo nimeyatoa, taarifa zinazosambaa katika

mitandao ya kijamii kwamba kampuni moja kutoka Saudi Arabia imepata mkataba wa uwekezaji wa kujenga na kuendesha Bandari ya Bagamoyo si za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kutokana na umuhimu, uzito na ukubwa wa programu ya hili Eneo Maalum la Kiuchumi la Bagamoyo, umma utajulishwa kikamilifu katika kila hatua ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kuwasilisha, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa ninamwita Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo mapema nimewasilisha katika Bunge lako Tukufu Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti kwa mwaka 2024/2025. Ninapenda kukushukuru kwa kuruhusu mjadala huu uliofanyika kwa weledi na viwango vya juu sana kama ambavyo mara zote Bunge lako Tukufu limekuwa likifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutambua kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa ushirikiano mkubwa ambao wameutoa katika maoni yaliyowasilishwa hapa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mpembenwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango na michango yote imekuwa ya kujenga ambayo inaashiria kazi kubwa ambayo ilishafanyika kwa ngazi ya Kamati. Michango hiyo tulikubaliana na Serikali inakubaliana nayo. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tumepokea maoni ya Kamati na maoni ya Waheshimwia Wabunge ambayo yamechangiwa katika Bunge lako Tukufu. Maoni haya yatafanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti hii ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kusisitiza kwamba *dedication* ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kushughulikia kero za Watanzania ni ya kiwango cha juu sana. Haya yameendelea kuonekana katika maelekezo yake na katika hatua anazozichukua na maelekezo yake ya fedha zote ziende kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo imeshafanyika na inaendelea kufanyika katika huduma za jamii ndiyo ambayo imetuweka Tanzania kuwa nchi ya juu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tunapokutana Mawaziri wa Fedha wa Afrika, Tanzania inaongoza katika utekelezaji wa miradi mingi sana. Tunaongoza katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Tanzania ni namba moja kwa nchi za *SADC*, *EAC* pamoja na nchi nyingine za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongoza katika utekelezaji wa miradi ya *P4R*, maji, mageuzi kwenye upande wa elimu na nishati kama ambavyo uliona juzi. Moja ya kigezo kilichotumika kuchagua nchi ya kupeleka *summit* (Kikao cha Wakuu wa Nchi) cha kutoa tamko lile kilifanyika hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongoza pia katika mageuzi ya kisasa kwenye sekta za uzalishaji. Bajeti iliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita kwenye upande wa sekta za uzalishaji haufananishwi na nchi yoyote katika kipindi hiki tunachopitia kwa wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ni sehemu tu ya baadhi ya ushahidi jinsi Serikali ya Awamu ya Sita ilivyoweka kipaumbele chake katika kuwatumikia Watanzania. Bila shaka Watanzania watairudisha Serikali hii madarakani katika uchaguzi ujao kwa kumpigia kura za kishindo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na mgombea mwenza wake, Dkt. Emmanuel Nchimbi ili kuweza kuhakikisha kwamba kazi hii kubwa inayofanyika inaendelea kutekelezwa, inakuwa endelevu na Tanzania kuweza kupiga hatua zaidi tunapoelekea kule mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea hoja hizo na kushukuru Bunge lako Tukufu, ninaomba sasa nitoe hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki na hii inaonesha namna Serikali hii ilivyofuata utawala bora. Jambo la kifedha lazima lipitishwe na Bunge, kwa hiyo hongereni sana Serikali. Pelekeni salamu kwa Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoendesha nchi kwa kufuata sheria za nchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Serikali (Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025) wa Mwaka 2025 *(The Supplementary Appropriation (For the Financial Year 2024/2025) Bill, 2025)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Serikali (Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025) wa Mwaka 2025**
***(The Supplementary Appropriation (For the Financial Year 2024/2025) Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Serikali (Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025) wa Mwaka 2025**
***(The Supplementary Appropriation (For the Financial Year 2024/2025) Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu, umetimiza hatua zote za Kibunge. Sasa nitawahoji; sasa Bunge lipitishe Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 wa Mwaka 2025 *(The Supplementary Appropriation (For the Financial Year 2024/2025) Bill, 2025)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa huu ni muswada rasmi umeshapitishwa na Serikali sasa imeshapewa kibali cha kutumia hizo pesa kwa idhini ya Bunge kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi yetu. Hongera sana Serikali kwa kutazama maeneo muhimu ambayo Waheshimiwa Wabunge waliiomba Serikali ifikirie kwenda kurekebisha na haya ndiyo mambo muhimu ambayo Waheshimiwa Wabunge mwende mkayaseme kwenye majimbo yenu. *(Makofi)*

Katibu.

## 14 FEBRUARI, 2025

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ninaomba kutoa taarifa kuwa shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge sasa zimemalizika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hoja ya Kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa fadhila zake zilizotuwezesha kufika siku hii muhimu ya kuhitimisha Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge la Kumi na Mbili tukiwa bukheri wa afya. Leo tunapohitimisha Mkutano huu hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuendelea kumuomba atujaalie afya ya kutimiza majukumu yetu kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Wakati wa kipindi chote cha Mkutano huu wa Kumi na Nane tumeshuhudia akiongoza mijadala yote kwa ukomavu wa hali ya juu. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa mafanikio ya mkutano huu yametokana na weledi mkubwa wa Mheshimiwa Spika wetu katika kusimamia shughuli za Bunge. Tufikishie salamu kwake kwa kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wake Spika wetu makini wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umechagiza Ofisi ya Bunge kupata Tuzo ya Mshindi wa Kwanza wa Taarifa Bora za Hesabu za mwaka 2023 iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania. Licha ya kutambua ubora wa taarifa iliyoandaliwa na Ofisi ya Bunge, tuzo hiyo inachagiza taasisi nyingine kuandaa taarifa za hesabu kwa viwango vinavyokubalika. Ninaipongeza sana Ofisi ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutumia nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge), Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Mbunge) na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika (Mbunge) kwa kazi kubwa ya kukusaidia katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge hili. Ninawapongeza sana kwa umahiri wao uliochangia shughuli za mkutano huu wa Bunge kuendeshwa kwa viwango vya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge pia yametokana na kazi kubwa iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge wote. Mijadala yote imekuwa na tija sana kwa Serikali na imechangia kufanya mageuzi makubwa katika utoaji huduma kwa wananchi pamoja na kurahisisha maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wake imekuwa ikifuatilia mijadala yote kwa makini na imepokea maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Kama ilivyo ada, itafanyia kazi michango yote iliyowasilishwa katika mkutano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa salamu za pongezi; katika Mkutano wa 74 wa Mawaziri wa Jumuiya ya Afya ya Kanda ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini uliofanyika Lilongwe, nchini Malawi, pamoja na mambo mengine ulifanya uchaguzi wa kumpata Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya hiyo. Uchaguzi huu ulifanyika baada ya aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya hiyo

kutoka Jamhuri ya Uganda kumaliza muda wake baada ya kuhudumu kwa miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchaguzi huo, Dkt. Ntuli Kapologwe - Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya Tanzania ambaye alikuwa akihudumua kama Mkurugenzi wa Afya Ustawi wa Jamii na Lishe, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi alikuwa mshindi wa nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya Nchi za Afrika za Mashariki, Kati na Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi huo, ulipatikana baada ya kuwashinda wagombea wengine sita waliokuwa wakiwania nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika tarehe 11 Februari, 2025. Hii ni kwa mara ya pili kwa Tanzania kushika nafasi hii katika kipindi cha miaka 51 cha Jumuiya hiyo, kwani kwa mara ya mwisho, Mtanzania Dkt. Winnie Mpanju Shumbusho alihudumu kama Mkurugenzi Mkuu kati ya mwaka 1993 na 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya hiyo inaundwa na nchi tisa wanachama ambazo ni Tanzania, Malawi, Zambia, Mauritius, Zimbabwe, Kenya, Uganda, Lesotho na Eswatini. Pamoja na nchi hizo, Jumuiya hii inafanya kazi katika nchi nyingine 23 Barani Afrika ambazo sio wanachama wa Jumuiya Hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuungana na Watanzania wote kumpa pongezi Dkt. Ntuli Kapologwe kwa kupeperusha bendera ya Taifa letu. Aidha, ninamtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya katika nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya Nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu za pole; tangu kuahirishwa kwa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge la Kumi na Mbili, wapo Watanzania waliokumbwa na majanga yaliyoleta athari mbalimbali zikiwemo vifo na uharibifu wa mali. Ninawapa pole Watanzania wote walioathirika kutokana na majanga hayo pamoja na wale waliopoteza wapendwa wao na mali zao. Kwa wale waliojeruhiwa nao ninawapa pole na ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka, Amina.

## 14 FEBRUARI, 2025

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 27 Novemba, 2024 Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani ukanda wa Afrika. Ninaendelea kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu Dkt. Ndugulile, amewahi kushika nafasi ya Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuanzia mwaka 2017 hadi 2020. Vilevile kuanzia mwaka 2020 hadi 2021 alishika nafasi ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, atakumbukwa kwa umahiri wake na michango yake wakati wa kipindi chote cha miaka 14 alichohudumu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninatoa pole kwa wanafamilia, Wana-CCM, wananchi wa Kigamboni, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Vilevile ninatoa pole kwa Jumuiya ya Kimataifa hususani Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 17 Desemba, 2024 Taifa letu liliondokewa na Mheshimiwa John Tendwa, Msajili Mstaafu wa Vyama vya Siasa. Marehemu John Tendwa atakumbukwa kwa kujenga misingi imara kwa vyama vya siasa. Pia atakumbukwa kwa ukomavu wake hususani katika kusimamia demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, tarehe 27 Desemba, 2024 tuliondokewa na Mheshimiwa Mwanaisha Athumani Kwariko, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi. Marehemu Mwanaisha Kwariko atakumbukwa kwa utumishi wake ndani ya mahakama na mchango wake mkubwa katika Tume Huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 Desemba, 2024 tuliondokewa na Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema aliyewahi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marehemu Jaji Fredrick Werema,

pamoja na kazi nyingine atakumbukwa kwa ushauri na mchango wake wa kisheria katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Watanzania wenzetu walipatwa na majanga baada ya jengo la ghorofa kuporomoka Kariakoo, Jijini Dar es Salaam. Tukio hilo lilisababisha athari mbalimbali ikiwemo vifo, uharibifu wa mali na miundombinu. Nami ninaungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa pole kwa Watanzania wote walioondokewa na ndugu, jamaa na marafiki pamoja na waliopoteza mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kutoa pole kwa majeruhi wote na ninamwomba Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka. Vilevile ninamwomba Mwenyezi Mungu awape marehemu wote pumziko la amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa Mkutano Mkuu wa Chama Tawala - CCM. Kipekee kabisa ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kufanikisha Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama cha Mapinduzi tarehe 18 na 19 Januari, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano huo, baada ya kuridhia na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 kama ilivyowasilishwa na Serikali ulifanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Vilevile ulifanya uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa CCM - Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wana-CCM wote kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wao ni kielelezo cha imani kubwa waliyoijenga kwa Wana-CCM wote inayotokana na uongozi wao makini. Hii ni heshima kubwa kwa viongozi wetu hawa na nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono ili waendelee kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi ana historia ndefu na uzoefu mkubwa ndani ya chama, Serikali na katika medani za kimataifa. Ninampongeza sana Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia kila la heri kwenye mchakato ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza Mheshimiwa Steven Masatu Wasira kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Bara. Sina mashaka nanyi mtakubaliana nami kuwa chama kimepata mtu sahihi kwa wakati sahihi kutokana na uzoefu wake na busara zake. Mheshimiwa Wasira ni kiongozi na mwanasiasa mkongwe ambaye mchango wake unaendelea kuhitajika katika kuimarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema mkutano ulipokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu hawa wamehakikisha kuwa matarajio ya Watanzania waliokipa dhamana Chama Cha Mapinduzi kuongoza Taifa hili yanatimizwa. Hakuna kata au shehia hata moja ambayo haijafikiwa kwa huduma muhimu kama yalivyo maelekezo ya Ilani

ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyosalia katika maeneo mengi ni ndogo na sina shaka utekelezaji wake utakamilishwa kwa wakati. Niwaombe Watanzania tuendelee kuwaunga mkono viongozi wetu kwa mustakabali wa maendeleo ya jamii nzima. Tuwaunge mkono kwani yajayo yanafurahisha sana katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Sote tumeshuhudia busara zake, weledi na umakini wa hali ya juu ambao amekuwa akiuonesha wakati wa kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, tumeshuhudia mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma kwa jamii. Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuwa kinara katika kusimamia mageuzi hayo ambayo pia yamegusa sekta zote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya mambo makubwa yanayostahili pongezi nyingi. Kama ulivyo usemi wa Kiswahili; "chanda chema huvikwa pete," Watanzania tuna deni kubwa kwa Rais wetu kwa namna ya pekee ya kulipa mema yote aliyoyatendea Taifa letu ni kwa kuendelea kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa anayoifanya inazidi kuonekana hapa nchini na hata nje ya mipaka ya nchi yetu. Kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakumbuka, tarehe 4 Februari, 2025, Dkt. Anita Zaidi, Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia kutoka Taasisi ya *Gates* alimkabidhi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuzo

maalumu ya Kimataifa ya *The Global Goalkeeper Award*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzo hiyo hutolewa mahsusi kwa viongozi ambao wameweza kuharakisha nchi zao kufikia malengo ya maendeleo endelevu kama ilivyo kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais amepewa tuzo hiyo kutokana na jitihada alizozifanya katika kupunguza viwango vya vifo vya wajawazito na watoto chini miaka mitano, lakini pia kukabiliana na tatizo la udumavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, viwango cha vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua kutoka vifo 556 mwaka 2015 hadi vifo 104 mwaka 2022 kwa kila vizazi hai 100,000. Idadi hiyo ni sawa na 80%. Hatuna budi sisi sote kumpa pongezi nyingi Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa watoto, vifo vimepungua kutoka vifo 67 mwaka 2015 hadi vifo 43 mwaka 2022 kwa kila vizazi hai 1,000. Idadi hiyo ni sawa na 35%. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii ya mafanikio, huu ni ushahidi kwamba Serikali inatoa huduma bora ambazo zimechangia kufikia viwango hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa watoto wachanga, Serikali imejiimarisha sana katika kutoa huduma, hivi sasa wodi maalumu za watoto wachanga zimeanzishwa katika hospitali 250 ikilinganishwa na wodi 14 zilizokuwepo mwaka 2018. Ni matarajio ya Serikali kuwa vifo vya watoto wachanga vitaendelea kupungua ifikapo mwaka 2030 na kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za dharura zimeimarishwa na zinapatikana katika maeneo mengi karibu na wananchi. Hivi sasa huduma za dharura zinapatikana katika vituo 116 vya kutolea huduma za afya kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na vituo saba vilivyokuwepo mwaka 2020. Uwepo wa huduma za dharura umechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hayo, bajeti ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa inaendelea kutengwa, miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya inaendelea kuimarishwa. Kadhalika, watumishi wa kada za afya wameendelea kuajiriwa ili kutoa huduma katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya. Jitihada hizo za makusudi zimekuwa chachu ya mafanikio ambayo yameangazia hadi nje ya mipaka ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa afua na mikakati inayotekelezwa hapa nchini, sina shaka utafiti utakaofuata utaonesha matokeo bora zaidi. Hali hii imetokana na jitihada za makusudi zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha huduma za afya hapa nchini ikiwemo huduma za mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pia amekuwa kinara katika mapambano dhidi ya udumavu. Jitihada na utashi wake umeifanya Tanzania kuwa mfano wa kuigwa na mataifa mengine kwa kuwa na mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka mtakubaliana nami kuwa suala la lishe limekuwa ajenda muhimu ya Mheshimiwa Rais, lakini pia jitihada zake za kuondoa udumavu hapa nchini zimeendelea kuonekana. Licha ya kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe, amekuwa kinara katika kuhakikisha jamii inajengewa uelewa kuhusu masuala ya lishe na kila mkoa unawajibika kushiriki katika utekelezaji wa afua za kukabiliana na ukosefu wa lishe iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtakumbuka, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisaini Mkataba wa Usimamiaji wa Lishe na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. Mkataba huo ulisainiwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na unalenga kuimarisha usimamizi wa huduma za lishe hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huo umeongeza pamoja na mambo mengine, mwitikio na uwajibikaji wa viongozi katika usimamizi na uratibu wa huduma za lishe nchini. Pia umeongeza kasi ya watoa huduma za lishe, hamasa kwa jamii na kupungua

kwa kiwango cha udumavu nchini kutoka 34% mwaka 2015 hadi 30% mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada za Mheshimiwa Rais, kati ya Julai na Septemba, 2023 Tanzania ilipewa heshima ya kuwa mwenyeji wa mikutano mikubwa ya kimataifa kuhusu lishe iliyofanyika Jijini Dar es Salaam. Mikutano hiyo ni pamoja na *Africa Human Capital Heads of State Summit* na *Africa Food Systems Forum 2023.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge la Kumi na Mbili, ulipokea na kujadili taarifa za mwaka kutoka kwa Kamati za Kudumu za Bunge, maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu ya Serikali, Miswada ya Sheria, sambamba na kujadili na kupitisha Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika *(Mission 300)* kwa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliuliza maswali 240 ya msingi na mengine 755 ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Halikadhalika, maswali 11 ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepokea miswada kumi ya sheria ambapo miswada mitatu ilisomwa kwa mara kwanza ambayo ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya *(The National Health Insurance Fund (Amendment) Act, 2025;* muswada wa pili ni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *(The National Housing Corporation (Amendment) Act, 2025;* na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2025).*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Bunge lako lilijadili na kupitisha miswada mingine saba kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024;

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi kwa Mwaka 2024;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024;

(vi) Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Maeneo Maalum ya Kichumi; na

(vii) Muswada wa Sheria Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 wa Mwaka 2025 *(The Supplementary Appropriation (For the Financial Year 2024/2025) Bill, 2025)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Serikali, umewasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuomba ridhaa ya Bunge ya nyongeza ya bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni 945.7 kwa kuwa fedha hizo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, fedha hizi zimeelekezwa kutekeleza shughuli za sekta ya elimu na afya, taasisi za utalii na utekelezaji wa programu mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kama ilivyoelezwa kwa kina na Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha muswada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili na kupitisha Azimio la Kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye

Mkutano wa Nishati wa Afrika *(Mission 300)* wa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitumie nafasi hii, kuungana na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupitisha Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wetu kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Afrika wa mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Asia Halamga ninanukuu; "Kipekee kabisa kwa kujidai ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikijivunia kuwa Mtanzania na kuongozwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe mwenye maono endelevu yanayolenga kuwanufaisha Watanzania wote, kiongozi wa mfano Barani Afrika na duniani kwa ujumla." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano huu ni sehemu ya fursa kubwa zinazozingatia nchi yetu kimataifa kutokana na ushawishi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na mkutano huu, nchi yetu imeongeza kasi ya kutangaza vivutio vya kitalii, kukuza diplomasia ya kiuchumi na kuimarisha taswira ya Tanzania kikanda na kimataifa. Sote tu mashuhuda mkutano uliratibiwa vizuri na kuleta sifa kubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kipekee, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa usimamizi wake mzuri na kwa maandalizi ya mkutano huo, amefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kila kilichopangwa kufanyika katika Mkutano wa Nishati Afrika kimefanyika kwa ufasaha, mafanikio na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninatoa pongezi kwa Wizara ya Nishati kwa uratibu wa mkutano huo. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaipongeza Kamati ya Makatibu Wakuu ikiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka na kamati hiyo ilifanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba mkutano huu unapata mafanikio. Hakika hawa wote wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepokea na kujadili taarifa 16 za Kamati za Kudumu za Bunge. Taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;

(ii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;

(iii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii;

(iv) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI;

(v) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria;

(vi) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Sheria Ndogo;

(vii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo;

(viii) Taarifa ya Kamati za Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;

(ix) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii;

(x) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira;

(xi) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma;

(xii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Bajeti;

(xiii) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(xiv) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo;

(xv) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Hesabu za Serikali; pamoja na

(xvi) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kamati ya Hesabu ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hizi muhimu zilizowasilishwa na Kamati zetu, tumeshuhudia mijadala mipana iliyojikita katika kuchangia maendeleo ya pamoja ya Taifa letu. Aidha, Serikali imepokea maoni yote na mapendekezo yenu Waheshimiwa Wabunge katika mkutano huu na ninaahidi kwamba Serikali itayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza maazimio ya Kamati zetu ninaziagiza Wizara zote kuandaa kwa wakati taarifa za maazimio yote kama yalivyowasilishwa na Kamati na kupitishwa na Bunge na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu ili kukamilisha taratibu za kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie maeneo mawili kwa kifupi ili kuhitimisha hotuba hii. Katika msimu huu wa 2020/2024 tunaingia kwenye msimu wa kilimo. Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea, mbegu bora na viuatilifu. Lengo la utoaji wa ruzuku hiyo, ni kupunguza gharama za mkulima ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, tunataka tuimarishe usalama wa chakula, lakini pia kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa pembejeo muhimu nchini ikiwemo mbolea na mbegu imeendelea kuimarika. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2024 kulikuwa na jumla ya tani 823,257 sawa na 82% ya makisio ya mahitaji ya tani milioni moja za mbolea kwa msimu huu wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mazao katika msimu huu wa kilimo inaendelea vizuri na mazao mengi yapo kwenye hatua mbalimbali za ukuaji, lakini vilevile baadhi ya maeneo yanayopata mvua za vuli, mazao yameanza kuvunwa hususani mahindi na maharage.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini inaeendelea kuwa nzuri. Katika msimu wa mwaka 2023/2024 uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani milioni 22.8. Kwa kuzingatia uzalishaji huo na mahitaji ya chakula cha tani milioni 17.7 kwa mwaka 2024/2025, nchi itakuwa na utoshelevu wa chakula wa 128%. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2025 Wakala imehifadhi jumla ya tani 776,000 za nafaka katika ghala za Wakala zilizopo kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kuwa baadhi ya maeneo nchini yanapata mvua chache, nitoe wito kwa wananchi kuchukua tahadhari mapema na kuzalisha mazao yanayokomaa kwa muda mfupi. Hatua hii iende sambamba na kutumia vizuri mavuno yaliyopatikana kwa kutunza chakula cha kutosha katika ngazi za kaya. Kadhalika, ninawakumbusha maafisa ugani kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wetu kuhusu mazao yanayostawi katika maeneo yao na uhifadhi wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni sekta ya elimu na mafunzo; tarehe 01 Februari 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023. Sambamba na sera hiyo, pia alizindua mitaala ya elimu ngazi ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya mitaala hiyo ni maono ya maelekezo ya Rais wetu yenye lengo la kufanya elimu inayotolewa hapa nchini iwiane na mahitaji ya sasa, lakini pia wahitimu wapate stadi na maarifa yatakayomudu mabadiliko na kasi ya ukuaji wa teknolojia. Vilevile wahitimu waweze kumudu ushindani katika soko la ajira kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pongezi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kukamilisha mapitio ya sera na

mitaala. Sera na mitaala hiyo imejikita katika kuwajengea ujuzi vijana wetu ili kuweza kuzalisha rasilimali watu yenye kukidhi mahitaji ya soko la ajira pamoja na stadi za karne ya 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa wadau wote wa elimu ikiwemo sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 ambayo ilianza kutekelezwa Januari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa sera na mitaala iliyoboreshwa, ninazielekeza mamlaka za mikoa, halmashauri na taasisi za elimu hapa nchini zijipange vizuri katika kuwezesha utekelezaji huo kwa ufanisi wa sera na mitaala hiyo kulingana na majukumu yao. Aidha, halmashauri ziweke kipaumbele katika kuanzisha na kuendesha shule za amali. Lengo ni kuwawezesha vijana wengi wapate ujuzi wa kuajiriwa au kujiajiri na hatimaye kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nieleze maeneo mawili madogo madogo; Maadhimisho ya Siku ya Wanawake. Tarehe 8 Machi Tanzania itaungana na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Mataifa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani itakayoadhimishwa kila mwaka hapa nchini. Hapa nchini, maadhimisho ya mwaka huu yaliyobeba kauli mbiu isemayo; "Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji" yanatarajiwa kufanyika kitaifa Jijini Arusha katika Viwanja vya Sheikh Amri Abeid. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya mwaka huu ni ya kipekee kwa sababu yatafanyika sambamba na kufikiwa miaka 30 ya utekelezaji wa Malengo ya Ulingo wa Beijing wa mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la maadhimisho hayo ni kutathmini na kutoa mrejesho kwa wananchi kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mipango, mikakati, miongozo, sheria na sera za kitaifa na kisekta kuhusu masuala ya usawa wa jinsia na uwezeshaji wananchi kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hii pia hutoa fursa kwa wananchi kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya jamii kushiriki shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Pia kutambua mchango wa wanawake katika kukuza usawa wa kijinsia na ustawi wa maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia tarehe 1 Machi, 2025 mikoa yote itafanya uzinduzi rasmi wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Maadhimisho ya mwaka huu yataambatana na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ili kuonesha kazi zinazofanywa katika nchi yetu kwa kipindi cha miaka 30 ya utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing 1995. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaelekeza wakuu wa mikoa yote nchini wakasimamie utekelezaji wa maadhimisho haya pamoja na kuhakikisha kwamba taarifa za utekelezaji zinawasilishwa kwenye Wizara yenye dhamana ya maadhimisho haya, lakini pia Waheshimiwa Mawaziri, wakuu wa taasisi, asasi za kiraia, sekta binafsi na wananchi wote kwa ujumla wajitokeze kwa wingi kushiriki kikamilifu kwenye maadhimisho hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili ni jambo la kitaifa ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kushiriki katika maadhimisho haya kila mmoja katika sehemu yake. Hii inatokana na ukweli kwamba mafanikio katika masuala ya kijinsia yanahitaji ushiriki wa kila mmoja katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maelezo mahsusi; ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu ninaomba kuweka msisitizo kuhusu maeneo hayo muhimu; la kwanza utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Nishati Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunakumbuka tarehe 27 hadi 28 Januari, 2025 nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika uliofanyika Jijini Dar es Salaam. Mkutano huu ulilenga kuhakikisha umeme unawafikia wananchi milioni 300 wa Bara la Afrika ifikapo mwaka 2030. Ili kuhakikisha maazimio ya Mkutano wa Nishati Afrika yanatekelezwa kikamilifu hapa nchini, na nchi yetu inanufaika, ninaelekeza yafuatayo:-

(i) Wizara zote zenye dhamana zihakikishe maazimio yote yaliyotolewa katika Mkutano wa Nishati wa Afrika yanatekelezwa ipasavyo;

(ii) Wizara ya Nishati yenyewe iendeleze kasi ya kuunganisha umeme nchini;

(iii) Wizara ya Nishati tena iweke mkakati wa kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme;

(iv) Wadau wote wa nishati safi ya kupikia waendelee kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuongeza kiwango cha matumizi ya nishati hapa nchini; na

(v) Kuongeza mchango wa sekta binafsi katika sekta ya nishati na yenyewe ishiriki kuhamasisha, lakini kusaidia kutoa vifaa vya kuendeshea shughuli za nishati safi ya kupikia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni udhibiti wa michango holela kwa wanafunzi waliodahiliwa. Msimu wa kuandikisha wanafunzi wa madarasa ya awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza unaendelea hivi sasa mikoa yote hapa nchini. Nitumie nafasi hii kuelekeza yafuatayo ili kutoa fursa kwa wanafunzi wote kujiunga na madarasa waliyopangiwa:-

(i) Wasimamizi wote wa elimu wazingatie katazo hili la Serikali kuhusu michango holela kama ilivyo kwenye Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2016. Waraka unabainisha majukumu ya wadau wote ikiwa ni pamoja na kuzingatia maelekezo ili kupata kibali cha mchango wa aina yoyote ile;

(ii) Licha ya waraka huo, wazingatie matamko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 ambayo pamoja na mambo mengine inatamka kuwa Serikali itahakikisha kuwa elimu ya awali, msingi na

sekondari inatolewa bila ada katika mfumo wa umma; *(Makofi)*

(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe wakuu wa shule zote wanatekeleza maelekezo haya ya Serikali ili watoto wote wa Tanzania wapate fursa ya kujiunga na masomo bila kikwazo cha gharama za michango. Suala hili lizingatiwe pia wakati wa udahili na wanafunzi nako pia jambo hili lizingatie, vilevile udahili wa wanafunzi wa kidato cha tano nako pia uzingatiwe; na

(iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa, wazazi, walezi, jamii na wadau wote wa elimu wahakikishe kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa wanajiunga na shule na asiwepo mwanafunzi atakayekosa fursa ya masomo kwa sababu ya michango holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo; mwaka 2024 ulikuwa ni mwaka wa mafanikio makubwa katika sekta ya sanaa, utamaduni na michezo. Hii imechagizwa na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba sekta hiyo muhimu hasa kwa vijana inakuwa na tija na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtakumbuka tarehe 14 Januari, 2025 Shirikisho la Soka Barani Afrika lilitangaza kuahirisha michuano ya wachezaji wa ndani wa Mataifa ya Afrika *(CHAN)* ambayo sasa itafanyika mwezi Agosti mwaka huu wa 2025. Uamuzi huo, kwa upande mmoja, unatupa sisi Watanzania nafasi ya kujiandaa vizuri zaidi kwenye mashindano kwa kuandaa miundombinu inayoweza kustahili kutumika kwenye mashindano haya. Vilevile inatupa nafasi kuhamasisha umma kujitangaza zaidi kwenye masoko ya utalii, uandaaji wa timu yetu ya Taifa na kwa upande mwingine kuvipa nafasi zaidi vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kujipanga kikamilifu kupokea wageni kutoka mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya michezo ikiwemo Kiwanja cha Arusha ambacho kwa sasa

kimefikia 26%. Vilevile tumeshuhudia tarehe 13 Februari, 2025 Serikali ikiingia makubaliano ya kimkataba na Kampuni ya *LIMONTA S.P.A* ya nchini Italy kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa kisasa hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika sekta ya michezo. Nitumie nafasi hii kupongeza kwa dhati kabisa kwa wanamichezo wote walioshiriki katika mashindano mbalimbali kitaifa na kimataifa na kuliletea heshima Taifa letu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza mwanariadha Magdalena Shauri kwa kuibuka tena kidedea katika mashindano ya *The Second Military All African Games* yaliyofanyika nchini Nigeria na mbio za Shenzhen zilizofanyika nchini China. Vilevile ninampongeza Alphonce Simbu kwa kuibuka tena kidedea katika mashindano ya mbio ya *The Second Military All African Games* yaliyofanyika Nigeria. Pia kwa kuibuka kuwa mshindi wa nne kwenye mbio za Valencia nchini Hispania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa masumbwi ninampongeza bondia Halima Vunjabei kwa kumpiga kwa *Knock Out* bondia Songul Ayten raia wa Uturuki anayeishi Ujerumani. Pambano hilo la Ubingwa wa Mabara *(WBF)* lilifanyika Novemba 23, 2024 nchini Ujerumani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninatoa pongezi kwa Bondia Kennedy Ayo kwa kumshinda Bondia Ismat Guliyev, raia wa Azerbaijan. Ushindi huo aliupata katika pambano la kimataifa lililofanyika tarehe 13 Desemba, 2024 nchini Urusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mpira wa miguu nianze kwa kuipongeza timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 17 *(Serengeti Boys)* kwa kufanikiwa kufuzu michuano ya *AFCON Under 17*. Kadhalika, timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 20 *(Ngorongoro Heroes)* kwa kufanikiwa kufuzu michuano ya *AFCON Under 20. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niipongeza timu ya Wanawake *(Twiga Stars)* kwa kufanikiwa kufuzu michuano ya Wanawake ya Afrika *(WAFCON)*. Licha ya hayo, ninaipongeza timu ya Taifa ya Tanzania *(Taifa Stars)* kwa kufanikiwa kufuzu Michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani *(CHAN)* na Michuano ya Mataifa ya Afrika *(AFCON)* 2025 itakayofanyika nchini Morocco. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niipongeze pia timu ya JKT *Queens* kwa kuwa mabingwa wa mashindano ya *CAF* ya Wasichana chini ya umri wa miaka 17 yanayofahamika *Girls Integrated Football Tournament*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushiriki wa vilabu vyetu kwenye Mashindano ya Kimataifa; awali ya yote niwapongeze viongozi wa *TFF* pamoja na Bodi ya Ligi Tanzania na wadau wa michezo kwa jitihada kubwa wanazozifanya na usimamizi mzuri wa ligi na mchezo wa mpira wa miguu kwa ujumla hapa nchi. *(Makofi)*

Nirudie kuwapongeza sana viongozi na wadau wote wa mchezo wa mpira wa miguu hapa nchini kwa ushiriki wao na kwa kuimarisha vilabu vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada hizo, Shirikisho la Kimataifa la Historia na Takwimu za Mpira wa Miguu limeitangaza Ligi Kuu ya Tanzania kuwa ligi ya nne kwa ubora Barani Afrika na kuwa ya 57 duniani kwa mwaka 2024. Kwa nafasi hiyo, ligi yetu imepanda kwa nafasi mbili zaidi kutoka nafasi ya sita mwaka 2023 ikizipiku Ligi za Afrika Kusini na Tunisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninavipongeza vilabu vyetu; *Dar Young Africans Sports Club* na *Simba Sports Club* kwa kumaliza hatua ya makundi ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Shirikisho. *(Makofi)*

Ninaipongeza sana *Simba Sports Club* kwa kuingia hatua ya Robo Fainali ya Kombe la Shirikisho. Ninaitakia kila la heri timu ya *Simba Sports* na mafanikio katika hatua inayofuata. Watanzania

tunalisubiri kwa hamu Kombe la Ubingwa wa Shirikisho hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaipongeza *Dar Young Africans Sports Club* kwa kuendelea kukonga mioyo ya Watanzania, kwa kuonesha umahiri katika mashindano mbalimbali. Kadhalika, ninawapongeza wanachama na mashabiki wote wa timu hiyo kwa kutimiza miaka 90 tangu kuanzishwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie; hapana siwezi kurudia kwa sbabu nimepongeza vilabu vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kushiriki kikamilifu katika mijadala yote kama ilivyoendeshwa katika kipindi chote cha Bunge hili. Kama nilivyotangulia kusema, michango yenu ni muhimu sana katika kuimarisha utendaji wa Serikali yetu na mimi niwapongeze kwa kuwatakia Waheshimiwa Wabunge safari njema, kurudi kwenye Majimbo yetu. Mkaendelee kuchapa kazi hasa huu mwaka wa 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Katibu wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuhakikisha kwamba ratiba iliyopangwa ya Mkutano huu inakamilishwa kwa mafanikio makubwa sana. Kadhalika ninavishukuru vyombo vya ulinzi na usalama. Hakika mmefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba usalama wa Waheshimiwa Wabunge na wageni wetu kwenye eneo hili kuwa ni ulinzi endelevu na hatimaye leo tunapohitimisha Mkutano huu tupo salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara zote au kwenye maeneo ya Serikali. Hakika mmefanya kazi kubwa na nzuri na mmekuwa mkitoa ufafanuzi unaohitajika kwa Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yanayogusa ufafanuzi na utendaji wenu umekuwa wa chachu ya

mafanikio ya mijadala ya hapa ndani ya Bunge kupitia Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuvishukuru vyombo vya habari vyote ambavyo vimekuwa vikihakikisha kila siku Watanzania wanapata habari kuhusu shughuli zote za Bunge letu hapa Dodoma. Ninawashukuru pia madereva wetu katika kipindi chote cha Mkutano huu mmeonesha nidhamu kubwa kabisa na utendaji wenye weledi na uaminifu mkubwa na mmetufikisha leo hii tukiwa salama na hatujapata taarifa ya ajali na matukio yale ambayo yanahusisha vyombo vyote vya moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zimebaki siku chache, waumini wa dini ya Kiislamu na Kikristo waanze ibada ya mfungo, niwatakie waumini wote ibada njema. Kipekee ninawatakia waumini wa Kiislamu maandalizi ya mfungo mwema wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani na waumini wa Kikristo, maandalizi ya mfungo mwema wa Kwaresma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hizo zote ni ibada muhimu kwa waumini wa madhehebu yote hayo ya dini, nitoe rai kwa wafanyabiashara wote nchini kutopandisha bei za vyakula kiholela. Wafanyabiashara wote mtambue ya kwamba mchango wenu ni muhimu katika kufanikisha ibada hizi. Ninawasihi sana endeleeni kushiriki katika ibada hizo kwa kurahisisha upatikanaji wa bidhaa muhimu wakati wa wote wa mfungo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Siku ya Jumanne tarehe 8 Aprili, 2025 Saa 3.00 Asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, ninakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaeni tu.

Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ripoti nzuri na sasa, nitawahoji. *(Kicheko)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki. *(Makofi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa kuna maelezo ya Spika kuhusu matukio muhimu kuelekea na wakati wa Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuungwa mkono na Wabunge, Mkutano ujao wa Bunge (Mkutano wa Kumi na Tisa) utaanza tarehe 8 Aprili, 2025. Kwa kuzingatia hilo, ninaomba niwapatie maelezo mafupi kuhusu matukio muhimu kuelekea na wakati wa Mkutano huo kama ifuatavyo:-

(i) Tarehe 10 Machi, 2025 Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge vitaanza. Aidha, Serikali itawasilisha kwa Katibu wa Bunge Nakala za Dondoo za Vitabu vya Bajeti pamoja na Randama za Makadirio hayo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Kanuni ya 115(1);

(ii) Tarehe 11 Machi, 2025 utafanyika Mkutano wa Wabunge wote ambapo Waziri wa Mipango na Uwekezaji atawasilisha mapendekezo ya Mpango wa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Waziri wa Fedha atawasilisha mapendekezo ya Serikali, kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kanuni ya 116(1) na (2);

(iii) Tarehe 12 Machi, 2025 Kamati za Kudumu za Kisekta zitaanza ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Kanuni ya 117(1);

(iv) Tarehe 19 Machi, 2025 Kamati za Kudumu za Kisekta zitaanza uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo. Kanuni ya 117(2);

(v) Tarehe 2 Aprili, 2025 Vikao vya Mashauriano kati ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali vitaanza kufikiria masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati zikijadili utekelezaji wa kazi wa Wizara. Kanuni ya 117(4), (5) na (6);

(vi) Tarehe 8 Aprili, 2025, Mkutano wa Bajeti utaanza rasmi;

(vii) Tarehe 12 Juni, 2025, inategemewa Bajeti ya Serikali itasomwa;

(viii) Tarehe 26 Juni, 2025, inategemewa Waziri Mkuu atatoa hotuba ya kuhitimisha Shughuli za Bunge la Kumi na Mbili; na

(ix) Tarehe 27 Juni, 2025, inategemewa Mheshimiwa Rais atalihutubia na kulifunga rasmi Bunge la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Wandengereko wanasema *wile mundu. (Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kifupi haya ndio matukio muhimu ambayo tunayatarajia wakati tunapohitimisha Bunge la Kumi na Mbili. Nimeyaeleza mapema ili muweze kupanga ratiba zenu vizuri na ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu kila mmoja apate kibali cha kushiriki katika Mkutano huo muhimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa katika kipindi hiki cha mapumziko katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, wenzetu Waislamu watakuwa kwenye mfungo wa mwezi Mtukufu wa

Ramadhani. Nitumie fursa hii kuwatakia mfungo mwema na Sikukuu njema ya *Eid El Fitr. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, sasa ninaahirisha Bunge mpaka tarehe 8 Aprili, 2025 saa 3.00 asubuhi, kama ilivyotamkwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

*(Saa 6.53 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne Tarehe 8 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*